# ILANI

## ACT WAZALENDO



TAIFA LA WOTE, MASLAHI YA WOTE.

ACT Wazalendo

2025 - 2030



# YALIYOMO:


SALAMU ZA KIONGOZI ........................................ i
HALI YA NCHI ........................................ iii
1. KUJENGA UCHUMI WA WATU NA WA KUJITEGEMEA UTAKAOZALISHA AJIRA MILIONI 12........................................1
1.1. AJIRA NA BIASHARA NDOGO NDOGO ........................................ 2
1.1.1. Kutoa Ajira kwa Vijana ........................................ 2
1.1.2. Kuwezesha Wafanyabiashara Wadogo na Wamachinga ........................................ 3
1.2. KILIMO, MIFUGO NA UVUVI ........................................ 4
1.2.1. Kufanya Mapinduzi Makubwa katika Kilimo ........................................ 4
1.2.2. Mifugo ........................................ 5
1.2.3. Uvuvi ........................................ 6
1.3. KUENDELEZA SEKTA YA VIWANDA ........................................ 7
1.4. UJENZI NA MAKAZI BORA ........................................ 9
1.5. SANAA, MICHEZO NA UTAMADUNI ........................................ 10
1.5.1. Sanaa ........................................ 11
1.5.2. Michezo ........................................ 11
1.5.3. Utamaduni ........................................ 12
1.6. KUIMARISHA SEKTA YA FEDHA, MIKOPO NA UWEZESHAJI WA WANANCHI........................................ 12
1.7. MAENDELEO YA SAYANSI, TEKNOLOJIA, UTAFITI NA UBUNIFU ........................................ 13
2. KUTOA HUDUMA BORA NA ZENYE STAHA ZA JAMII KWA WOTE ........................................ 15
2.1. AFYA BORA KWA WOTE ........................................ 16
2.2. KUTOA ELIMU BORA, BURE KWA WOTE ........................................ 20
2.2.1. Elimu Msingi ........................................ 20
2.2.2. Elimu ya Juu ........................................ 22
2.2.3. Elimu ya Ufundi........................................ 22
2.3. MAJI SAFI NA SALAMA KWA WOTE ........................................ 23
2.4. NISHATI ........................................ 24
2.5. HIFADHI YA JAMII KWA WOTE ........................................ 25

2.6. HUDUMA BORA ZA MAWASILIANO NA UHURU WA HABARI ........................ 27
3. KUBORESHA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA UCHUKUZI ........................ 28
4. KUSIMAMIA HAKI, USAWA, DEMOKRASIA NA USALAMA WA RAIA .................... 31
4.1. KATIBA MPYA .................................................................................................. 32
4.2. KUPAMBANA NA RUSHWA NA UFISADI ............................................................ 33
4.3. KUREKEBISHA MFUMO WA SHERIA NA UPATIKANAJI HAKI ........................ 34
4.4. KUHAKIKISHA ULINZI NA USALAMA WA RAIA.................................................. 36
4.5. KUBORESHA MASLAHI NA UTENDAJI WA WATUMISHI WA UMMA ............. 36
4.6. WANAWAKE, WAZEE NA WATU WENYE ULEMAVU ....................................... 39
4.6.1. Kuongeza Ushiriki wa Wanawake katika Uongozi na Maendeleo................ 39
4.6.2. Kuwatunza na Kuwaenzi Wazee ..................................................................... 40
4.6.3. Kushirikisha Watu wenye Ulemavu ................................................................. 40
5. KULINDA NA KUSIMAMIA ARDHI NA RASILIMALI ZA TAIFA ................................. 41
5.1. UPATIKANAJI, MATUMIZI NA ULINZI WA ARDHI KWA WANANCHI .............. 42
5.2. MADINI, MAFUTA NA GESI ............................................................................... 44
5.3. MISITU, BAHARI NA UHIFADHI ........................................................................ 46
5.4. KUKUZA UTALII ................................................................................................ 47
6. KUIMARISHA MUUNGANO NA MAHUSIANO YA KIMATAIFA ................................ 49
6.1. KUIMARISHA MUUNGANO ............................................................................... 50
6.2. UMOJA WA AFRIKA NA UHUSIANO WA KIMATAIFA ....................................... 51
KULINDA MAZINGIRA NA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI ....... 52



# SALAMU ZA KIONGOZI



ACT Wazalendo

Ndugu Watanzania wenzangu,
Nchi yetu imetimiza na kuvuka miaka 60 ya uhuru na kujitawala. Leo hii tulipaswa kusheherekea na kuenzi miaka 60 ya uhuru kwa kuonesha ukomavu wa maendeleo ya taifa na watu wake. Miaka 60 iilipaswa kutokomeza kabisa maisha ya fedheha, dhiki na dhahama. Miaka 60 ilipaswa kutoa majawabu dhidi ya changamoto za kijamii, kisiasa na dhidi ya udumavu wa kiuchumi. Miaka 60 ilipaswa kutoa tumaini la kweli kwa wananchi wote kuyaishi maisha bora, yenye staha na ya haki.

Miaka 60 ilipaswa kutufanya tuwe taifa na watu wenye nguvu na ushawishi wa kijamii, kisiasa, kiuchumi na hata kiteknolojia. Miaka 60 ilipaswa kutufanya kuwa nchi kinara barani Afrika na kutuweka kwenye nafasi kuu katika ramani ya ulimwengu. Miaka 60 ilipaswa kutufanya tuwe nchi yenye kheri, neema na baraka tele. Lakini miaka 60 na zaidi imekuwa miaka si kitu.

Kama taifa tumeshindwa vita tuliyoitangaza dhidi ya adui Umasikini, Maradhi na Ujinga. Katika kipindi cha miaka mitano (2020 – 2025), tumeshuhudia kiwango cha watu wanaoishi kwenye umasikini wa kutupwa kikiongezeka maradufu, kutoka watu milioni 12 hadi watu milioni 24. Hivi sasa, umasikini umekuwa si jambo la ajabu tena; umasikini umekuwa ni hali ya kawaida, unaonekana dhahiri na wala haushtui. Serikali haisumbuliwi tena kuona watu wake wakionesha hali zao duni na dhohofu hadharani.Hivi sasa tumejikabidhi na tumejenga urafiki na adui umasikini.

Hii leo, huduma za afya zimekuwa hujuma za afya! Wagonjwa wamekuwa — watejall na wamegeuzwa mtaji wa fedha; vituo vya afya na hospitali zimegeuzwa kuwa vijiwe vya upatu. Leo hii, uhai umefanywa bidhaa; kujifungua kumekuwa mradi wa wauguzi; na hospitali zimegeuka soko la kuuza watoto. Pasipo haya, hadi kifo nacho kinapigwa mnada, maiti zimefikiwa, nazo zinapigwa bei. Hivi leo, maradhi si adui tena, ni swahiba! Miaka 60 ya uhuru bado watoto wetu wanaketi chini; bado janga la walimu ni kubwa kuliko linavyoelezwa; bado huduma ya maktaba na maabara ni ndoto; bado shule zinafanywa kambi za wakimbizi kwa wanafunzi kubebeshwa vyakula, maji na kila aina ya mizigo ya kutweza utu na utoto wao.

Miaka 60 badala ya kukabiliana na ujinga, tumeamua kuupamba; tumeamua kusheherekea wahitimu wa shule za msingi wasiojua kusoma na kuandika; tumeamua kuwa na wahitimu wa sekondari wasioweza kufikiri na kujitegemea; tumeamua kuwa na wasomi wa vyuo vikuu wasioweza kujieleza na kujisimamia. Tumeamua kuusimika ujinga kwenye tambo za madarasa matupu na tumeamua kuuficha ujinga kwa kuuvisha magauni shahada za uzuzu. Hivi sasa, ujinga si adui tena, tumeutokomeza kwa kugawa vyeti kama njugu.

Mapambano yaliyoasisiwa na wazee wetu, wake kwa waume, yamesalitiwa, yamepuuzwa, yamewekwa kapuni. Mapambano yaliyolenga kunusuru watu wa nchi hi kutoka kwenye makucha ya unyonyaji, ukandamizaji na udhalili, uliosababishwa na utawala wa kikoloni, yametelekezwa. Mapambano ya kuhakikisha nchi hii inaongozwa na kuwanufaisha wakulima na wafanyakazi yamezimwa na genge la wahuni wachache.i Mapambano ya kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya haki, usawa na uhuru yamenajisiwa na walafi wa madaraka.

Nchi yetu imechukuliwa na kuwekwa mateka na mafisadi wanaoitwa viongozi; na vibaka wa haki wanaohubiri amani; na wahuni wanaosisitiza uzalendo; na makuwadi wanaoitwa waheshimiwa; na watesi wanaojidai wacha Mungu; na wachache wanaojivika utukufu. Nchi yetu imegeuzwa danguro la upigaji na ubadhirifu wa mali za umma; danguro la uporaji wa ardhi na rasilimali asili kwa manufaa ya wachache; danguro la udangaji wa mikopo na madeni yasiyo na tija.

Ule Mwenge ―uliowekwa juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike hata nje ya mipaka yetu; ulete tumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo mahali palipo na chuki na heshima palipojaa dharau,‖ hivi sasa umezima. Haujazima kwa upepo au kukosa nguvu, bali umezimwa na serikali ya CCM. Miaka 60 baadaye, nchi yetu inashuhudia watu wake, wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara, wachimbaji, wasanii ma wafanyakazi kwa ujumla, kutokuwa na matumaini; inashuhudia chuki na hofu kutamalaki; nchi yetu inashuhudia utu kutwezwa, heshima kubezwa na dharau kuenezwa.

Watanzania wenzangu, tuna jukumu la kihistoria na kimapambano kusimama nakukataa udhalili na udhalimu wa serikali ya Chama cha Mapinduzi. CCM wametudhihirishia kwamba hawana tofauti yeyote ya msingi na wakoloni weupe. Na kama tulivyotangaza vita dhidi ya mkoloni mweupe, hatuna budi kutangaza vita dhidi ya CCM, kwa kuwa wametuonea kiasi cha kutosha, wametunyonya kiasi cha kutosha na wametupuuza kiasi cha kutosha! Miaka 60 ya unyonge uliotufanya tuonewe, tunyonywe na tupuuzwe na CCM inatosha!

Chama chetu cha ACT Wazalendo kimedhamiria kuibeba azma na jukumu hili la mabadiliko ya kweli na mapinduzi dhidi ya mfumo mbovu na dumavu wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tumedhamiria kuiongoza vita ya kulitoa Taifa letu katika hali ya unyonge na kulitia katika hali ya nguvu; vita vya kuwafanya wananchi wa Tanzania (na wananchi wa Afrika) watoke katika hali ya dhiki na kuwa katika hali ya neema. Ilani hii tamko letu, ahadi yetu, kiapo chetu na nadhiri yetu kwa Watanzania.

Tumedhamiria kurejesha thamani na heshima ya utu wetu. Tumedhamiria kuiondoa nchi yetu kutoka kwenye makucha na magenge ya wahuni wachache. Tumedhamiria kuirejesha nchi yetu katika misingi ya haki na katika maamuzi ya Watanzania. Tumedhamiria kuhakikisha Tanzania inakuwa, Taifa la Wote, Kwa Maslahi ya Wote!



Ndg. Dorothy Jonas Semu
Kiongozi wa Chama
ACT Wazalendo



# HALI YA NCHI

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Tanzania imepitia mabadiliko makubwa yenye athari hasi kwa maisha ya watu, ustawi wa taifa na mwelekeo wa kisiasa wa nchi yetu. Serikali ya CCM imeshindwa kusimamia ipasavyo uchumi, huduma za jamii, na masuala ya utawala bora. Watanzania wengi wanaishi katika umaskini, ukosefu wa ajira na uhakika wa vipato; Watanzania wengi wanaishi wakiwa hawana huduma bora za kijamii, wanaiishi kwa hofu, wakizuiwa kupaza sauti na kupewa matumaini hewa ya kesho iliyo njema. Wakati viongozi na wahuni wachache wakijivunia kuwa Watanzania, Watanzania wengi wanavumilia kuwa Watanzania. Tumeendelea kuwa taifa la wachache kunufaika na walio wengi kuteseka.

Uchumi wa taifa unatajwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.1 kwa mwaka (BoT, 2025), lakini ukuaji huo haujafanikiwa kutengeneza ajira zenye staha, kutoa kipato cha uhakika wala unafuu wa maisha kwa wananchi. Zaidi ya vijana milioni 3.5 hawana ajira kabisa, huku walio katika ajira wengi wao wakiwa katika sekta isiyo rasmi inayohusisha wakulima, wafugaji, wavuvi, wamachinga, bodaboda na wengine. Vijana hawa wanaishi bila hifadhi ya jamii, kipato cha uhakika, mishahara mizuri au usalama wa kazi.

Asilimia 65 ya Watanzania hutegemea kilimo, mifugo na uvuvi kwa maisha yao. Hata hivyo, bajeti ya maendeleo katika sekta ya kilimo haijawahi kufikia kiwango cha 10% kilichowekwa na azimio la Maputo. Ufugaji unakosa malisho, maji na masoko. Wavuvi wanakandamizwa kwa tozo, vibali na ukosefu wa zana. Ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji na kuhifadhi mazao unasababisha mazao kuharibika au kuuzwa kwa bei ya chini. Serikali imeshindwa kuunganisha sekta hizi na viwanda vya kuongeza thamani. Wakulima wanauza mazao yao kwa bei ya hasara, bila masoko ya uhakika, huku pembejeo zikiwa za gharama kubwa na zisizo na ubora.

Wafanyakazi na watumishi wa umma wanalipwa mafao kidogo baada ya miaka ya kazi ngumu, huku mfumo mzima wa hifadhi ya jamii ukiwa dhaifu, kandamizi na usiotoa matumaini kwa wastaafu wa sasa na baadaye.

Deni la Serikali limeongezeka kwa kasi hadi kufikia zaidi ya shilingi trilioni 107.7 mwaka 2025, ikiwa ni ongezeko la zaidi ya shilingi trilioni 54 ndani ya miaka mitano pekee. Serikali imegeuza mikopo kuwa chanzo kikuu cha uendeshaji wa bajeti badala ya mapato ya ndani. Ongezeko la kasi la deni linaweka mzigo mzito katika mabega ya wananchi wa kawaida na kutishia uhuru wa nchi na kufanya uchumi unaondeshwa kwa deni.

Wakati huo huo, zaidi ya asilimia 86 ya Watanzania waliopo kwenye sekta isiyo rasmi hasa wanawake, vijana na wazalishaji wadogo au wafanyabiashara wadogo wanakutana na masharti magumu na riba kubwa ya hadi asilimia 40 kwa mwezi kutoka taasisi za mikopo binafsi. Hakuna mfumo wa kitaifa wa fedha unaowasaidia kupata iii mikopo nafuu, bima ya afya, au huduma za hifadhi ya jamii. Mfumo wa sasa wa fedha unaendeshwa kwa faida ya wachache hasa mabenki, wafanyabiashara wakubwa na tabaka la juu la watawala. Tanzania ina rasilimali nyingi kama vile madini, gesi, mafuta, misitu na wanyamapori lakini hazijanufaisha vya kutosha taifa. Kati ya mwaka 2016 na 2025, sekta ya madini imekuwa ikichangia wastani wa asilimia 5 tu kwenye Pato la Taifa licha ya kuwa na dhahabu, almasi, tanzanite, na madini mengine ya kimkakati. Ufisadi, mikataba mibovu na ukosefu wa uwazi katika mapato ya serikali vimefungua

milango ya upotevu wa mapato (illicit financial flows). Takwimu za Global Financial Integrity zinaonesha Tanzania inapoteza zaidi ya Shilingi trilioni 2 kila mwaka kwa njia ya utoroshaji wa rasilimali, ukwepaji kodi unaofanywa na kampuni za kimataifa na mikataba isiyo na tija. Vile vile, Tanzania imekumbwa na wimbi la uporaji wa ardhi za wakulima na wafugaji kwa kisingizio cha uwekezaji na uhifadhi wa mazingira, hali iliyoibua migogoro mikubwa ya ardhi na ukiukwaji wa haki za binadamu. Ma-elfu na ma-laki ya wananchi wameondolewa kwenye ardhi zao bila ridhaa wala fidia stahiki, huku serikali dhalimu ikichukua ardhi zao kwa kutumia vyombo vya dola na dhulma kubwa; wakipigwa, kuchomewa nyumba, kutaifishiwa mifugo au kutimuliwa kwa mabavu. Mfumo wa sasa wa umiliki wa ardhi unawapora wananchi haki yao halali na kuwageuza wakimbizi (manamba) katika nchi yao wenyewe.

Huduma za jamii kama afya, elimu, maji, makazi, na hifadhi ya jamii zimeendelea kuwa duni, zenye upendeleo, zisizowafikia masikini na watu walioko pembezoni na vijijini. Wakati Serikali inazungumza juu ya bima ya afya kwa wote na elimu bure, hali halisi ni kwamba wananchi wanaendelea kulipa fedha kupata huduma hizo, au hukosa kabisa huduma.

Katika afya, bajeti ya taifa imeendelea kuwa chini ya asilimia 3 ya bajeti kuu kwa miaka mitano mfululizo – mbali kabisa na kiwango kilichoazimiwa kwenye Azimio la Abuja la asilimia 15. Takriban asilimia 40 ya vituo vya afya havina dawa muhimu, na ni chini ya asilimia 10 ya Watanzania walio na bima ya afya. Watanzania 600,000 huingia kwenye umasikini kila mwaka kutokana na gharama za matibabu.

Katika elimu, madarasa yamejaa kupita kiasi – shule zenye zaidi ya wanafunzi 150 kwa mwalimu mmoja si nadra. Watoto wa familia masikini wananyimwa elimu bora kwa sababu ya ada fiche, michango, uhaba wa walimu, na mazingira duni ya kusomea. Takwimu zinaonesha zaidi ya watoto milioni moja kila mwaka hukatisha masomo kabla ya kumaliza elimu ya msingi.

Zaidi ya asilimia 55 ya Watanzania hawana uhakika wa kupata maji safi na salama kila siku. Katika miji, takwimu zinaonesha wastani wa asilimia 42 ya maji yanayozalishwa hupotea kutokana na miundombinu chakavu. Katika maeneo ya vijijini, mamia yaiv wanawake na watoto wanatembea zaidi ya kilomita 5 kila siku kutafuta maji. Miji mingi imejaa makazi holela na haina miundombinu ya majitaka wala maji ya mvua. Nishati pia imekuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo ya watu. Ni asilimia 30 tu ya Watanzania waliounganishwa na umeme wa gridi ya taifa, huku vijiji 481 nchini havina kabisa huduma hiyo. Umeme unakatika mara kwa mara na sio wa uhakika na gharama za kuunganisha umeme zimekuwa kubwa. Kodi za vifaa vya nishati jadidifu ni kubwa na hakuna motisha kwa wananchi kutumia nishati mbadala. Vyanzo mbadala vya nishati vimewekwa kando licha ya utajiri mkubwa wa jua, upepo na jotoardhi.

Miundombinu ya usafiri na uchukuzi ni duni mno nje ya miji mikubwa. Barabara nyingi za vijijini hazipitiki wakati wa mvua, zikiwa na mashimo na bila madaraja. Wakulima wameshindwa kusafirisha mazao yao, wakina mama wajawazito kufika hospitali, na wanafunzi kufika shule. Hakuna reli inayounganisha kanda ya kusini wala maeneo yenye migodi ya kimkakati kama Mchuchuma na Kabanga. Utawala wa sheria, haki za binadamu na demokrasia vimeporomoka. Vyombo vya dola vimekuwa silaha za kisiasa. Viongozi wa upinzani wamepigwa, kutekwa, kubambikiwa kesi au kuuawa. Matukio ya watu kupotezwa yamekuwa ya kawaida bila uchunguzi wala uwajibikaji. Serikali imejenga utawala wa hofu, usaliti na vikwazo dhidi ya ushiriki wa raia.

Tanzania inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi kama ukame, mafuriko na kushuka kwa tija ya kilimo, hali inayoathiri zaidi wakulima, wafugaji na wavuvi vijijini. Ongezeko la shughuli za kibinadamu—ukataji miti, ujenzi holela, na matumizi ya kemikali

viwandani—limeharibu mazingira na kuhatarisha afya za wananchi. Wakati huo huo, miradi mipya ya biashara ya hewa ya ukaa (carbon trading) inachipua bila miongozo madhubuti ya kulinda haki za wananchi wanaoishi katika maeneo ya misitu.

Baadhi ya mikataba ya biashara ya kaboni inawaondoa watu kwenye ardhi yao ya jadi au kuwanyima fursa ya kuitumia kwa maisha yao ya kila siku—bila fidia wala ushiriki. Hili linaongeza dhuluma kwa jina la mabadiliko ya tabianchi. Serikali haijawekeza vya kutosha katika utabiri wa hali ya hewa, mifumo ya tahadhari na miundombinu ya kukabiliana na majanga.

Wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu wameendelea kubaki nyuma katika mfumo wa maamuzi na fursa. Wamachinga wanakandamizwa mijini, wakulima wanatozwa ushuru hadi kwa mazao wayawekayo nyumbani, wafugaji wanauawa kwa migogoro ya ardhi, wavuvi wanapigwa kwa tozo na masharti yasiyoeleweka.

ACT Wazalendo tunakuja na matumaini mapya. Tunatambua kwamba taifa linaweza kuongozwa kwa haki, uwazi, na misingi ya ushiriki wa wananchi kikamilifu. Tumedhamiria kujenga Taifa la Wote kwa Maslahi ya Wote. Taifa ambalo kila Mtanzania, popote alipo, anaweza kuishi kwa heshima, kupata huduma bora, kufanya kazi kwa uhuru na kunufaika na rasilimali za nchi yake.

Ilani hii inabeba maono ya kuijenga Tanzania mpya – Taifa la Wote kwa Maslahi ya Wote. Taifa ambalo watoto wote wanapata elimu bora bila kulipishwa, wala kuchangishwa. Taifa ambalo kila mwananchi anapata huduma ya afya bila kuingia kwenye umasikini. Taifa ambalo wakulima, wafugaji, wavuvi na wamachinga wanatambuliwa, kuheshimiwa na kuwezeshwa. Taifa ambalo sheria ni sawa kwa wote na itasimamia haki. Taifa ambalo serikali inawajibika kwa wananchi, na uhuru wa maoni unalindwa. Taifa ambalo serikali itashiriki kikamilifu katika uchumi na uzalishaji wa ajira kwa vijana. Taifa ambalo wazee na watu wote wanapata hifadhi ya jamii na wanaishi kwa wakati wote maisha yenye staha na heshima.

ACT Wazalendo imedhamiri kufanya yafuatayo:

- Kujenga uchumi wa watu utakaozalisha ajira milioni 12 kwa kufufua viwanda,kupunguza tozo na kuongeza uzalishaji wa kilimo.
- Kuhakikisha huduma bora na za staha kwa wote, zitakazopatikana bila ubaguzi na kwa utaratibu rafiki kwa kila Mtanzania. Tutahakikisha elimu bure hadi chuo kikuu, afya kwa wote kupitia bima ya afya iliyofungamanishwa na mfumo wa hifadhi jamii, na upatikanaji wa maji na nishati kwa gharama nafuu.
- Kujenga taifa lenye haki, usawa na kidemokrasia, kwa kurejesha mchakato wa katiba mpya, kulinda utu na usalama, kuondoa rushwa, na kujenga serikali yenye `uwazi na uwajibikaji.
- Kuboresha na kupanua miundombinu ya usafiri, reli, barabara na nishati, kuhakikisha ufikiwaji wa huduma na kuchochea maendeleo ya uchumi.
- Kulinda na kusimamia ardhi, mazingira na rasilimali kwa maslahi ya wananchi wote. Tutapitia mikataba ya madini, mafuta, gesi na misitu; na kukomesha uporaji wa ardhi. Tutahakikisha rasilimali asili zinakuwa mtaji wa kutukomboa kutoka kwenye lindi la umasikini.
- Kuimarisha muungano na kuufanya kuwa muungano wa haki, usawa na wenye kuheshimiana, kwa kuhakikisha kila upande unakuwa na mamlaka kamili kwa mambo yasiyo na muungano. Na kuirejesha hadhi ya Tanzania katika ramani na diplomasia ya kimataifa.
- Kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, huku tukilinda uhuru wetu, pasipo kuigeuza nchi yetu kuwa shamba la kuhalalisha uchafuzi wa mataifa yaliyoendelea, huku sisi tukibaki na uchumi dumavu na tegemezi.

# 1.KUJENGA UCHUMI WA WATU NA WA KUJITEGEMEA UTAKAOZALISHA AJIRA MILIONI 12



Kwa taifa kuwa na uchumi imara, unaokua na endelevu ni lazima uchumi huo utokane na watu wenyewe kupitia shughuli zao za kilimo, uvuvi, ufugaji, viwanda, uvunaji wa rasilimali, utalii, biashara na biashara ndogondogo n.k. Uchumi wa kujitegemea usiotegemea mikopo na misaada kufanya shughuli za maendeleo na kuleta ustawi wa watu. Uchumi wa watu utakaolinda heshima na uhuru wa taifa ni uchumi unaozalisha ajira za kutosha kwa wananchi na kuzalisha mapato mengi kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani.

Dhamira yetu ni kujenga uchumi wa watu, unaojitegemea; uchumi utakaozalisha ajira mpya milioni 12 ndani ya miaka mitano, kwa kukuza shughuli zinazoajiri watu wengi na kuongeza pato la taifa na pato la mtu mmoja mmoja na thamani bidhaa. Tunataka uchumi mkubwa wa serikali utakaokua kufikia uchumi wa kati wa juu kufikia 2030; na tunataka maendeleo hayo ya kiuchumi yasiache wananchi mamilioni katika umasikini na ufukara kwa kukosa kazi za staha.

Serikali yetu haitaacha Watanzania kuwa watazamaji na washangiliaji wa shughuli za maendeleo bali itaweka uchumi mikononi mwao. Itabadili kabisa mfumo wa sasa wa kutajirisha wachache na kufukarisha wengi. Katika kufikia dhamira hii Serikali ya ACT Wazalendo itajikita katika sekta zifuatazo

# 1.1. AJIRA NA BIASHARA NDOGO NDOGO



### 1.1.1. Kutoa Ajira kwa Vijana

Ili kukabiliana na ukosefu wa ajira nchini na kuondokana na umasikini, serikali ya ACT Wazalendo inalenga kutengeneza taifa linalofanya kazi (a working nation) na itafanya hivyo kwa kutengeneza ajira mpya za staha milioni 12 ndani ya miaka mitano, kwa kuchukua hatua zifuatazo:

i. Itatengeneza ajira mpya milioni 2.8 zitakazotokana na viwanda ndani ya miaka mitano (5) ya uongozi wa ACT Wazalendo. Hili litawezekana kwa kuchukua hatua zifuatazo:
   a. Itafufua na kutoa msukumo wa makusudi wa ujenzi wa viwanda vipya na kuboresha uendelezwaji wa viwanda vilivyopo, haswa viwanda vinavyogusa sekta ya kilimo na kutoa vivutio vya viwanda vichanga.
   b. Itaanzisha maeneo maalum ya viwanda na biashara (special economic zones) yatakayoanzisha viwanda vikubwa vyenye uwezo wa kuajiri watu wasiopungua elfu ishirini (20,000), katika kanda saba: Kanda ya Kusini, Kanda ya Juu Kusini, Kanda ya Kati; Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kati, ili kuongeza ajira kwa vijana nchini kote.
   c. Itatunga sheria itakayohakikisha na kuweka utaratibu wa asilimia 80 ya bidhaa vitu na huduma zinazotumika kwenye miradi/ shughuli za ujenzi na maendeleo za serikali zinatumia malighafi na bidhaa za ndani, hususani zinazotoka katika eneo husika, ili kufungamanisha na mnyororo wa thamani.

ii. Itatengeneza ajira zenye staha zisizopungua laki tatu kwenye soko la sanaa, michezo na utamaduni kwa kuweka mifumo mizuri ya kisera na uwekezaji.

iii. Itaimarisha ubora na kutafuta soko la nje kwa kazi za ubunifu kama uhunzi, uchongaji, uchoraji na bidhaa zingine zitokanazo na kazi za mikono.

iv. Itaondoa mfumo wa zabuni katika taasisi za umma, kwenye huduma za ulinzi,usafi, ukarabati wa vifaa na majengo ili kuziongezea uwezo taasisi hizo kutoaajira rasmi na zenye staha kwa watu wengi.

v. Itaajiri wahitimu wote wa kada za ualimu, afya na kilimo na kuweka utaratibu wa kuajiri kila mwaka wahitimu katika sekta hizi.

vi. Itajenga na kuimarisha uwezo wa mashirika ya umma na taasisi za serikali kujiendesha kwa tija na faida ili kuongeza ajira.

vii. Itapunguza kodi ya wafanyakazi (PAYE) ili kuwaongezea wafanyakazi kipato waweze kumudu mahitaji katika maisha, kujiwekea akiba au kuanzisha na kuendesha shughuli za uzalishaji kipato cha ziada.

viii. Itatengeneza mazingira mazuri ya kisera na kisheria yatakayowezesha vyama vya wafanyakazi kuwa huru, imara na kusimamia maslahi ya wafanyakazi kwa ufanisi.

ix. Itarejesha mfumo wa ukokotoaji wa mafao unaomnufaisha mstaafu kulipwa kwa mkupuo asilimia 50.

x. Italipa malimbikizo yote ya madeni stahiki ndani ya kipindi cha miaka miwili.

### 1.1.2. Kuwezesha Wafanyabiashara Wadogo na Wamachinga

Mfumo wetu wa uchumi umetoa fursa ya kundi kubwa la watu kujihusisha na biashara ndogo ndogo. Kwa kutambua nafasi ya wafanyabiashara wadogo wadogo, wamachinga bodaboda na kwa kutambua changamoto makundi haya wanayopitia ya unyonyaji na ukandamizaji, serikali ya ACT Wazalendo tutafanya yafuatayo:

i. Italinda haki za wafanyabiashara wadogo kwa kuruhusu kwa utaratibu kufanya biashara katika maeneo ya miji na yenye mkusanyiko wa watu katikati ya miji, vituo vya mabasi, kando ya barabara na pembeni ya majengo ya umma, kwa kutunga sheria ndogo ndogo

ii. zitakazowapa wamachinga hadhi ya kisheria ili kulinda shughuli zao na kuboresha mazingira ya biashara.

iii. Itazingatia, katika ujenzi wa miundombinu mipya mijini, inatenga maeneo kwa ajili ya wamachinga.

iv. Itapiga marufuku serikali kutumia vyombo vya dola na mgambo kuwahamisha, kuwabughudhi, kuwavunjia, kuwanyanyasa na kupora mali za wafanyabiashara wadogo.

v. Itaweka utaratibu utakaoondoa unyonyaji kwa bodaboda wanaochukua vyombo vyao kwa mikataba.

vi. Italinda, kuondoa usumbufu wa polisi kwa bodaboda na kuweka mazingira rafiki yatakayopunguza ajali na kuwawezesha ili kukukuza ustawi wao.

vii. Itawaunganisha wafanyabiashara wadogo katika mfumo wa hifadhi ya jamii (NSSF) kuwawezesha wapate mikopo, bima ya afya na kinga dhidi ya ajali na majanga.

viii. Itaanzisha na kuimarisha masoko maalum kwa siku, masaa au mwezi mahususi kwaajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo na wajasiriamali.

# 1.2. KILIMO, MIFUGO NA UVUVI



### 1.2.1. Kufanya Mapinduzi Makubwa katika Kilimo

ACT Wazalendo inatambua kuwa kilimo ndio shughuli kuu ya uchumi. Tunatambua wakulima kama watu muhimu katika upatikanaji wa chakula, uzalishaji wa ajira na maendeleo ya watu. Kukua na kuimarika kwa sekta ya kilimo kutasaidia kukua kwa sekta ya viwanda, mifugo na biashara na kubadili kabisa maisha ya mamilioni ya Watanzania.

Dhamira yetu ni kufanya mapinduzi ya kilimo na kuifanya sekta hii ikue kwa asilimia 8 kwa mwaka na kuongeza mavuno mara mbili zaidi kwa eneo la uzalishaji na kuhakikisha kilimo kinabadili maisha na maeneo yao. Kufikia hayo, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itatenga na kuwekeza asilimia 20 ya bajeti ya maendeleo kwenye sekta ya kilimo, hii ikiwa ni maradufu ya lengo la Umoja wa Afrika kupitia Mpango Kamili wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP).

ii. Itafungamanisha sekta ya kilimo na sekta ya viwanda, ili kuhakikisha angalau asilimia 85 ya malighafi ya viwanda vya ndani inatokana na wakulima wa ndani.

iii. Itatoa ruzuku na nafuu kwa ajili ya wakulima na vyama vya ushirika kuanzisha na kufufua viwanda vidogo vya kuchakata mazao vijijini.

iv. Itapanua kilimo cha umwagiliaji hadi kufikia hekta milioni 2 na kutoa msisitizo kwenye matumizi ya nishati jadidifu, hususani sola, ili kukuza kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabia nchi.

v. Itawekeza katika uhifadhi, uzalishaji na usambazaji wa mbegu asilia na kupiga marufuku matumizi ya mbegu zilizobadilishwa vinasaba maabara (genetically modified seeds - GMO).

vi. Itawekeza angalau shilingi bilioni 150 kwa mwaka katika utafiti, uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora, na kuongeza mnyororo wa thamani kwa mazao yote ya kimkakati.

vii. Itajenga maghala ya nafaka na majokofu ya kuhifadhi mazao baridi (cold rooms) katika kila wilaya na mkoa wa Tanzania bara na visiwani.

viii. Itaboresha mfumo wa malipo ya mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi, ikiwemo stakabadhi ghalani, na kufanya uwe wa malipo ya papo kwa papo, kwa njia ya kidigitali.

ix. Itaimarisha mfumo wa taarifa ya bei za mazao na kutafuta masoko ya uhakika ilikuondoa unyonyaji wa watu wa kati kwenye mazao ya kilimo.

x. Itajenga na kuimarisha miundombinu ya masoko na kuweka mfumo wa usimamizi wa masoko wa ubia kati ya wakulima, wafanyabiashara na serikali.

xi. Itahimiza na kuwezesha matumizi ya mbinu za kilimo cha kiikolojia, kulinda afya, ardhi na mazingira na kuhakikisha upatikanaji wa chakula salama.

xii. Itapunguza na kuondoa ushuru wa mazao unaokandamiza wakulima wadogo nchini.

### 1.2.2. Mifugo

Shabaha yetu ni kuinua sekta ya mifugo, kurejesha heshima kwa wafugaji na kuongeza mapato ya nchi na wananchi. Tanzania, kama nchi ya pili kwa idadi ya ng`ombe barani Afrika, inapaswa kutosheleza mahitaji ya mazao ya mifugo kama maziwa, nyama na ngozi na kunufaika na soko kubwa la nje. Katika kuendeleza sekta ya mifugo na wafugaji, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itatenga maeneo maalumu kwa wafugaji, na kuwekeza katika miundombinu ya maji na malisho ili kumaliza migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

ii. Itawekeza kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo kama nyama, maziwa na ngozi ili kuongeza thamani na ajira.

iii. Itawezesha wafugaji kupata soko la uhakika na bei nzuri kwa bidhaa za mifugo kupitia mamlaka maalumu ya sekta.

iv. Itakuza mifumo jumuishi ya kilimo na ufugaji ili kuongeza tija, kipato na matumizi bora ya ardhi.
v. Itapanua huduma za bima ya mifugo na mikopo rafiki kwa wafugaji ili kulinda uzalishaji dhidi ya majanga na kuongeza mtaji.

vi. Itaongeza na kuendeleza kitaaluma maafisa ugani wa mifugo, pamoja na kuwapatia vifaa vya kisasa vya kuwahudumia wafugaji.

vii. Itatengeneza uhusiano wa karibu kati ya vyuo vya kilimo, biashara, jamii na ufundi kwa ajili ya uvumbuzi na uendelezaji wa mifugo.

### 1.2.3. Uvuvi

Serikali ya ACT Wazalendo itawafuta machozi wavuvi wa Tanzania, itaboresha na kuheshimu kazi hii na kuziwezesha kuwa salama na endelevu. Katika kukuza sekta ya uvuvi na wavuvi itate keleza yafuatayo:

i. Itaondoa tozo na taratibu kandamizi, ikiwemo leseni za wavuvi.

ii. Itawekeza na kujenga katika maghala baridi na masoko ya kisasa ya samaki katika mikoa na wilaya zote za uvuvi.

iii. Italinda haki za wavuvi wadogo kwa kuwashirikisha na kuondoa vikwazo katika matumizi ya bahari, mito na mabwawa.

vi. Itaanzisha mfuko maalum wa ruzuku kwa ajili ya viwanda vya usindikaji wa mazao ya uvuvi.

vii. Itatenga angalau bilioni 50 kwa mwaka kuwekeza kwenye miundombinu ya kusaidia uvuvi wa bahari kuu.

viii. Itapanua huduma za kifedha kwa wavuvi, ikijumuisha mikopo na bima ya mazao ya uvuvi ili kuwajengea uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, kununua vifaa vya kisasa vya uvuvi na vya kuhifadhia mazao ya uvuvi.

ix. Itawezesha upatikanaji wa zana na teknolojia rafiki kwa mazingira kwa ajili ya uvuvi ende levu na kuongeza kipato cha wavuvi.

x. Itatunga sheria zitakazo toa ulinzi na uhuru wa wavuvi kuuza mazao yao ndani na nje ya nchi kwa utaratibu rafiki.

xi. Itaimarisha ushirikiano wa vyuo vya uvuvi na taasisi za masoko ili kukuza utaalamu wa uvuvi wenye tija.

xii. Itawezesha uwekezaji kwenye bandari za uvuvi Tanga, Kigoma, Nyasa, Mwanza na Mafia ili kunufaika na uvuvi mkubwa wa maziwa na bahari kuu.

# 1.3. KUENDELEZA SEKTA YA VIWANDA



Dhamira yetu ni kuwa na nchi ya viwanda - vitakavyozalisha ajira na kuchakata malighafi na kuziongeza thamani mazao. Ni jukumu la serikali kufungamanisha sekta ya viwanda na malighafi za ndani na kuongeza uwezo wa ndani wa uzalishaji. Ili kufikia dhamira hii, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itapiga marufuku kuuza malighafi nje ya nchi isipokuwa pale tu ambapo uwezo wa ndani wa kuzalisha bidhaa za mwisho ni mdogo, ili kulinda ajira na kuongeza thamani ndani ya nchi.

ii. Itatoa kipaumbele kwa viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kupunguziwa gharama za uzalishaji kama umeme, maji, kodi na huduma za usafirishaji, kwa kutoa ruzuku kwa viwanda vinavyochipukia.

iii. Itafufua viwanda vya kuchakata pamba na kuzalisha nguo (textile), kwa lengo la kuunda ajira mpya zaidi ya 1,000,000 kupitia zao la pamba.

iv. Itawezesha ujenzi wa viwanda vya zana za kilimo, viuatilifu, mbolea na teknolojia za kisasa, kwa kushirikiana na taasisi za utafiti na makampuni ya kimataifa, lengo

v. likiwa ni kuajiri vijana wasiopungua 500,000.Itatumia na kuboresha mahusiano ya kikanda kuongeza mauzo ya bidhaa kama mazao ya kilimo, vifaa vya ujenzi n.k. mara mbili ya kiwango cha sasa kwa kuimarisha ushindani wa viwanda vya ndani.

vi. Itawezesha ujenzi wa viwanda vidogo vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika vya wakulima vijijini ili kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, na kuzalisha ajira katika ngazi ya jamii.

vii. Itashiriki moja kwa moja katika umiliki wa viwanda vya msingi kama vile vya chuma cha pua, kwa ajili ya kuweka msingi thabiti wa viwanda vya kati na vidogo.

viii. Itaandaa na kutekeleza mpango maalumu wa kuhamisha viwanda na teknolojia kutoka nchi zilizoendelea kuja Tanzania ili kuijengea nchi uwezo, ujuzi na teknolojia ya uzalishaji.

ix. Itawezesha uanzishaji wa maabara za kisasa na viwanda vya ubunifu wa teknolojia kwa kushirikiana na taasisi za ndani na za kimataifa, ili Tanzania iwemzalishaji wa teknolojia, siyo soko tu.

# 1.4. UJENZI NA MAKAZI BORA



Ili kuwa na jamii yenye heshima, ustawi na staha, makazi bora ni jambo la lazima. Gharama kubwa kwenye sekta ya ujenzi kuanzia vifaa, ujenzi na maeneo ni miongoni mwa vikwazo vikubwa kwa wananchi na kwa sekta nzima. Serikali ya ACT Wazalendo itasimamia na kushirikisha wadau kuhakikisha Watanzania wanaishi kwenye nyumba za staha na ujenzi unakua nafuu kwa kufanya yafuatayo:

i. Itatenga maeneo na kushirikiana na serikali kuu na wadau wengine kujenga nyumba za gharama nafuu kwa watumishi wa umma katika kila mkoa.

ii. Itasimamia ujenzi wa nyumba laki tano (500,000), katika maeneo mbali mbali, kwa ajili ya watumishi wa umma, wazee, watu wenye ulemavu pamoja na watu wenye hali duni.

iii. Itaanzisha vyama vya ushirika wa makazi mijini na vijijini, vitakavyosaidia wakulima, wafanyabiashara na wajasiriamali kumiliki makazi bora kupitia mikopo na hifadhi ya jamii.

iv. Itakamilisha upimaji wa miji yote nchini ili wananchi waweze kuishi kwenye maeneo yaliyopangwa na yenye huduma muhimu za kijamii.

v. Itashirikiana na taasisi za kifedha kuwezesha vikundi vya vijana mafundi ujenzi kuanzisha miradi ya makazi nafuu ya gharama ndogo.

vi. Itaandaa mpango maalum wa kuboresha makazi duni mijini (slums upgrading), ili kila Mtanzania aishi kwenye makazi salama, ya kiutu na yenye huduma za msingi.

vii. Itahakikisha ulinzi wa wapangaji wa kipato cha chini dhidi ya unyonyaji wa kodi na ukosefu wa usalama wa makazi.

viii. Itawekeza katika mifumo ya kuondosha maji ya mvua kwenye miji ili kupunguza mafuriko, kwa kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa na kitaifa.

## 1.5. SANAA, MICHEZO NA UTAMADUNI



Sanaa, michezo na utamaduni sio tu sekta za burudani bali ni ajira, kichocheo cha uchumi, amani, mshikamano na utambulisho wa jamii. Sekta hii inakua kwa kasi sana lakini wasanii, wanamichezo na wanautamaduni, hasa wazawa, hawanufaiki vyakutosha. Tunataka kukuza zaidi sekta hii na kuona vipaji na vipawa vya Watanzania na hali yetu ya kinchi, kihistoria na kijiografia vinasaidia kukuza sekta hii na kunufaisha wananchi na taifa. Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

### 1.5.1. Sanaa

i. Itahakikisha ulinzi wa kazi za sanaa ndani na nje ya nchi, hususani kazi za muziki na filamu, kwa kuimarisha uwezo wa kisheria na vyombo vya kiserikali kusimamia kazi hizo; na kwa kuboresha mahusiano na wasanii na jumuiya za sanaa kimataifa.

ii. Itatoa na kusambaza elimu ya haki za wasanii na biashara ya sanaa ili kuhakikisha ulinzi wa kazi na maslahi ya waandishi.

iii. Itajenga kumbi 6 za kisasa za sanaa na burudani (arenas) katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Mtwara; na itashirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujenga kumbi moja kubwa na ya kisasa kwa upande wa Zanzibar, ili kukuza uchumi wa burudani.

iv. Itashirikiana na waandishi na vyama vya waandishi ili kuimarisha uwekezaji na kuboresha maslahi katika sanaa ya uandishi.

v. Itashirikisha wadau wote katika ukokotoaji, ukusanyaji na mgawanyo wa mirabaha ya kazi zote za ubunifu, hususani muziki na filamu.

vi. Itatenga maeneo mahususi kwa ajili ya uhifadhi (gallery) na kuweka utaratibu maalum wa maonesho ya kazi za sanaa ya uchoraji, ufumaji, uchongaji na uhunzi.

vii. Itatenga bajeti maalumu kusaidia wasanii chipukizi kupata mitaji na mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kukuza na kuendeleza vipaji vyao.

vii. Itafungamanisha na kuboresha mahusiano ya sekta ya michezo na burudani na sekta ya utalii na mambo ya nje ili kuongeza uchumi wa kitaifa, ajira na mapato ya fedha za kigeni.

### 1.5.2. Michezo

i. Itahakikisha ujenzi wa shule za michezo (sports academies) katika kanda nnenchini, kwa kushirikiana na halmashauri, mashirika ya umma na sekta binafsi.

ii. Itasimamia ujenzi wa viwanja vipya na matengenezo na uendelezaji wa viwanja vya michezo vilivyopo kwa kushirikiana na halmashauri za serikali za mitaa.

iii. Itatoa motisha kwa kampuni na watu binafsi wanaowekeza kwenye timu au miundombinu ya michezo watapewa msamaha wa kodi kwa gharama za uendeshaji zinazotumika kukuza michezo.

iv. Itaanzisha mifumo ya bima kwa wanamichezo na kuhakikisha uwepo wa utaratibu ende levu wa matunzo ya kiafya ili kuboresha maslahi ya wanamichezo.

v. Itasimamia uwepo wa vyombo huru na makini vya wanamichezo vitakavyosimamia maendeleo ya michezo na wanamichezo.

vi. Itatenga na kurejesha viwanja vyote vya michezo ambavyo vimeporwa kutoka kwa umma na kuhakikisha uwepo wa viwanja bora katika kila mtaa, kijiji na kitongoji.

### 1.5.3. Utamaduni

i. Itakarabati na kuendeleza maeneo ya kihistoria na kiutamaduni, sambamba na kutenga maeneo ya wazi kwa ajili ya shughuli za kijamii na mapumziko.

ii. Itafungamanisha sekta ya utamaduni na sekta ya utalii na kuziwezesha kibajeti Halmashauri ili kukuza utalii vijijini.

iii. Itatenga bajeti maalum kwa ajili ya kuwezesha utafiti, uandaaji wa vipindi na programu mbali mbali za kiutamaduni na kutunza taarifa zinazohusiana na utamaduni wetu.

# 1.6. KUIMARISHA SEKTA YA FEDHA, MIKOPO NA UWEZESHAJI WA WANANCHI




Katika kipindi cha miaka mitano, deni la taifa limeongezeka kwa takribani trilioni 50, hadi kufikia zaidi ya trilioni 104. Pamoja na ongezeko hili maradufu la deni linalozidi kulididimiza taifa kwenye dimbwi la utegemezi; taifa linakabiliwa na changamoto ya utoroshaji wa fedha na ukwepaji mkubwa wa kodi unaoigharimu taifa zaidi ya trilioni 1 kwa mwaka. Wakati uchumi wa kitaifa ukiendelea kufubazwa, wananchi nao wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa mtaji na utitiri wa madeni ya mikopo umiza, yenye riba kubwa.

Ili kukabiliana na changamoto ya kifedha, mtaji na mikopo, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itaongeza mtaji kwa benki ya ushirika na kuimarisha huduma zake kwa wananchi.

ii. Itawezesha Hifadhi ya Jamii kusaidia wananchi kupata mikopo ya gharama nafuu.

iii. Itasimamia sheria na kudhibiti utoaji wa mikopo yenye riba kandamizi kulinda wananchi dhidi ya watu na taasisi zinazotoa mikopo kandamizi.

iv. Itaanzisha mfuko wa mikopo kwa vijana na wanawake wenye ubunifu hasa walioko kwenye teknolojia.

v. Itafuta misamaha yote ya kodi isiyo rafiki katika uchumi wa nchi na kudhibiti ukwepaji na utoroshaji wa fedha nje ya nchi.

vi. Itatunga sheria kali dhidi ya ukwepaji wa kodi na utoroshaji wa fedha nje ya nchi.

vii. Itaimarisha mabenki ya jamii na ushirika ili ziweze kutoa huduma kwa wananchi wengi na kwa gharama nafuu.

viii. Kutathmini upya mikataba ya kikanda na ya kibiashara ya kifedha ili iwe na manufaa kwa Taifa.

ix. Itaifufua na kuimarisha benki ya DCB kwa kuiongezea mtaji na kuiwekea mfumo wa kutumika kukusanya mapato na malipo yote katika Jiji la Dar es Salaam.

x. Itahamasisha matumizi ya vikundi vya kijamii vya kuwezeshana na kuviwekea mifumo mizuri na rafiki, ya kisheria na kisera, ya kuvilinda.

## 1.7. MAENDELEO YA SAYANSI, TEKNOLOJIA, UTAFITI NA UBUNIFU



Dunia inakwenda kwa kasi sana, Tanzania na nchi nyingi za Afrika zimekua walaji wa sayansi na teknolojia na si wazalishaji, licha ya malighafi zote zinazotumika katika teknolojia hizo kupatikana. Bado sekta ya uzalishaji na huduma zinatumia teknolojia ya zamani inayochukua muda mrefu na gharama kubwa. Haya ni kutokana na nchi kutokua na mipngo thabiti inayotekelezwa katika eneo la sayansi, utafiti na ubunifu. Serikali ya ACT Wazalendo inalitazama eneo hili kama kitovu cha ufanisi na muunganiko wa dhati wa dunia; inataka kuiweka Tanzania katika ramani ya juu ya sayansi, teknolojia, utafiti na ubunifu itakayosaidia kurahisisha shughuli za watu na matumizi ya rasilimali na malighafi kuzalisha bidhaa bora na zinazokwenda na wakati, kwa kufanya yafuatayo:

i. Itaanzisha Mpango Mkakati Maalum wa Kitaifa utakaokuwa na jukumu la kutafuta, kutambua na kuendeleza wabunifu.

ii. Itaanzisha Miji Maalum ya Ubunifu na Wabunifu, vitakavyotenga maeneo maalum, kwa ajili ya kuzalisha na kuendeleza shughuli za ubunifu.

iii. Itatoa ruzuku, mikopo na vivutio vya kodi kwa watu na makampuni yanayofanya ubunifu wa kiteknolojia unaolenga kuboresha shughuli za uzalishaji na upatikaji wa huduma za kijamii.

iv. Itahakikisha ulinzi wa ubunifu wa ndani na mawazo ya kibunifu [intellectual property] kwa kuimarisha sera na sheria za ubunifu.

v. Itaimarisha uratibu na usimamizi wa shughuli za sayansi, teknolojia na ubunifu; na kufungamanisha moja kwa moja shughuli hizo na shughuli za uzalishaji na upatikanaji wa huduma za kijamii.

vi. Itaweka utaratibu bora utakaowezesha kubadilishana kwa ujuzi, maarifa na uzoefu wa kisayansi na teknolojia, na wadau na mataifa mbalimbali.

vii. Itaimarisha mfumo wa usimamizi, uratibu na mashirikiano kati ya serikali na sekta binafsi, katika shughuli za ubunifu.

viii. Itahakikisha asilimia 2 ya pato la taifa inatengwa na inatumika kwa ajili ya shughuli za utafiti na maendeleo.

ix. Itaanzisha vituo vikubwa vya utafiti na maendeleo katika kanda 3, na kuzifungamanisha na shughuli za kanda husika.

x. Itabadili na kuboresha sera na sheria ya utafiti na kurudisha uhuru wa wanataaluma na watafiti katika kuzalisha na kukuza fikra za ukombozi.

xi. Itatoa ruzuku, mikopo na vivutio vya kikodi katika utekelezaji wa tafiti zinazolenga kushughulika na majanga na changamoto/ matatizo sugu katika jamii.

# 2. KUTOA HUDUMA BORA NA ZENYE STAHA ZA JAMII KWA WOTE



Serikali ya ACT Wazalendo imedhamiria kujenga Tanzania yenye huduma bora, nafuu na za staha kwa watu wote, na inatambua kuwa huduma bora kwa wote ndio msingi wa maendeleo ya watu. Dhamira yetu ni kuwa na jamii yenye afya bora, isiyo na ubaguzi ambayo Watanzania wote wanapata huduma bora na kuwa na afya bora; jamii ya watu walioelimika kwa kuwa na maarifa yanayoendana na wakati na mahitaji ya jamii; jamii yenye uhakika wa maji safi na salama nyumbani; jamii yenye umeme wa uhakika kwa kila kaya pamoja na huduma nyengine. Hii ndio jamii tunayoimaanisha tunaposema,Taifa la Wote, Maslahi ya Wote!

# 2.1. AFYA BORA KWA WOTE



Serikali ya ACT Wazalendo inaamini kwamba, huduma bora za afya ni haki ya asili ya binadamu, na hivyo ni haki ya msingi ya kila Mtanzania, bila kujali hali na kipato chake. Tunatambua kwamba magonjwa hayachagui tajiri wala masikini na hayana muda maalumu, hivyo ni lazima taifa liwe na mfumo bora wa kimatibabu kwa wote kwa wakati wote; lazima tuwe na mfumo unaozingatia usawa na ubora katika upatikanaji wa huduma ya afya kwa wote na wakati wote.

Serikali ya ACT Wazalendo itatoa huduma bora za afya kwa wote kwa kufungamanisha mfumo wa bima ya afya na hifadhi ya jamii kwa wote. Kupitia mfumo huu, zaidi ya Watanzania milioni 18 watakua wanachama wa mfuko hifadhi ya jamii ambao utahakikisha watu wote wanapata matibabu bora, si kulingana na vipato vyao bali kulingana na magonjwa au mahitaji yao. Katika kufikia shabaha hii serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

### 2.1.1. Uongozi Bora, Uwazi na Uwajibikaji katika Sekta ya Afya

Kwa kuzingatia kwamba afya ni haki ya msingi kwa ustawi na maendeleo ya watu, Serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha kwamba wananchi wanakuwa katika sehemu ya maamuzi na usimamiz wa sekta hii, ili kuongeza uwajibikaji na ufanisi wa serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora na bure za afya kwa wote na kwa wakati wote. Hivyo, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itaongeza ushirikishwaji wa jamii: Itaanzisha kamati rasmi [Kamati za Afya za Wananchi – KAAWA] katika kila kata, zisizofungamana na chama chochote cha siasa, ili kushiriki katika upangaji wa bajeti, ufuatiliaji wa ubora wa huduma na uandaaji wa mipango ya kujikinga na magonjwa.

ii. Itaweka mfumo wa kuthibiti ubora wa huduma za afya: Itatumia viashiria vya kitaifa (Quality Indicators) na mfumo wa maoni ya wagonjwa mtandaoni, ili kuweka hadharani ripoti za ubora wa huduma za afya.

### 2.1.2. Mfumo wa Kugharamia Huduma za Afya

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itaanzisha Bima ya Afya ya Taifa kwa Wote kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mfumo huu utahakikisha kila Mtanzania anapata huduma bure na bora, kwa huduma zote zaafya na wakati wote, kupitia bima ya afya iliyounganishwa na mfumo wa hifadhi ya jamii.

ii. Itagharamia bajeti ya sekta ya afya kwa asilimia 100 na kuondoa utegemezi wa wahisani katika sekta ya afya, ikiwa ni pamoja na kuongeza bajeti ya afya hadi asilimia 15 ya bajeti kuu kulingana na Azimio la Abuja.

iii. Itapiga marufuku tozo/ ada ya maiti na gharama za matibabu kwa waliofariki, kwa kuweka sheria ya kuzuia hospitali za umma kudai gharama za matibabu kwa mgonjwa aliyefariki.

### 2.1.3. Upatikanaji wa Huduma Bora na Salama za Afya kwa Wananchi

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itajenga wa zahanati mijini na vijijini kufikia lengo la kuwa na zahanati 1 kwa watu 1000.

ii. Itajenga hospitali kubwa tatu za kanda zenye hadhi, uwezo na viwango vya kimataifa,
iii. katika mikoa ya Mara, Ruvuma na Singida.

iv. Itaimarisha Mfumo wa Dharura (EMS) kwa kuhakikisha upatikanaji wa gari za kisasa za wagonjwa katika ngazi ya afya ya msingi, namba ya dharura na wahudumu wakwan za (community first-responders) wenye mafunzo kwa kila kata.

v. Itaimarisha huduma za mama na mtoto kwa kuboresha miundombinu ya huduma ya mama na mtoto, katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya; na kusimamia upatikanaji wa huduma hizo bila malipo, wala michango yeyote ile.

vi. Itakuwa marufuku wajawazito kutakiwa kwenda kujifungua na vifaa vya kujifungua.

vii. Itaweka mtaalamu wa afya ya akili kwa kila hospitali ya wilaya, na kuanzisha programu za huduma za kisaikolojia, na ushauri kwa njia ya mtandao na kwenye ngazi ya zahanati na vituo vya afya.

viii. Itaanzisha programu za ushauri wa kisaikolojia mashuleni na vyuoni kote.

ix. Itadhibiti na kupambana na magonjwa sugu kama vile ukimwi, kifua kikuu, ukoma, saratani, figo, na kisukari, kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya upimaji, chanjo na tiba bure kuanzia ngazi ya zahanati na vituo vya afya.

x. Itatokomeza kabisa ugonjwa wa malaria na kuangamiza mazalia ya mbu nchini kote, hususani kupitia kampuni ya kitaifa ya Tanzania Biotech Products Limited (TBPL).

xi. Itaimarisha na kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za kibingwa kwenye hospitali zote za wilaya.

xii. Itaanzisha Mpango wa Chakula Shuleni (School Feeding Programme) na ufuatiliaji wa ukuaji kwa kutumia kadi za kidigitali. Itahakikisha kila mtoto anapata lishe bora kwa ajili ya ukuaji na kupata kinga bora ya mwili.

xiii. Itatoa huduma za afya kwa usawa bila ubaguzi. Itatoa elimu na kusimamia utekelezaji wa sheria, sera na kanuni zinazohakikisha huduma sawa kwa wote, bila kujali umri, magonjwa au uwezo wa kifedha, katika hospitali zote za umma.

xiv. Itatoa elimu endelevu kwa umma kwa kuratibu vipindi vya TV/Redio, mitandao ya kijamii na kampeni mashuleni na mitaani, kuhusu kinga za magonjwa, lishe bora na afya ya akili.

### 2.1.4. Wafanyakazi wa Sekta ya Afya

Katika kutengeneza nguvu kazi yenye motisha na ujuzi katika sekta ya afya vijijini na mijini, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itaajiri na kuwawezesha wataalamu wawili wa afya (Me&Ke) katika kila kitongoji, ili kuratibu na kufuatilia mienendo ya afya kwa kaya, mitindo ya maisha, viashiria vya magonjwa na kutoa elimu ya afya.

ii. Itaongeza mishahara kwa asilimia ishirini (20%) na kuimarisha maslahi ya watumishi katika sekta ya afya ili kutoa motisha zaidi kujiunga na kubaki hospitali za umma.

iii. Itaajiri wahudumu wapya wa afya 500,000 katika kipindi cha miaka mitano, ikiwa] ni pamoja na madaktari, manesi, wataalamu wa maabara, wanasaikolojia pamoja na wataalamu wengine, ili kumaliza uhaba wa wahudumu wa afya.

iv. Itachagua wanafunzi wa fani za afya kutoka maeneo ya vijijini na kuwapa ufadhili (scholarship) na mafunzo kwenye vyuo vya afya kwenye kanda zao, kwa masharti ya kufanya kazi kwenye maeneo yao kwa kipindi maalumu baada ya kuhitimu (rural bonding).

i. Itaweka kifurushi cha motisha kwa wafanyakazi wa afya vijijini, kitachojumuisha mishahara ya juu, nyumba, ufadhili wa masomo ya juu, fursa za kupanda vyeo,na tuzo za kutambua mchango wao, ili kuhamasisha wafanyakazi wa afya wafanye kazi vijijini (Bundled incentives).

ii. Itapanua vyuo vya afya kwa kila kanda na kuanzisha programu za mafunzo kwa vitendo vijijini ―rural internship‖ zenye posho.

### 2.1.5. Tafiti za Afya

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itaongeza bajeti kwa ajili ya tafiti za afya kwa wataalam na taasisi za afya kwa zaidi ya asilimia 50 kwa kipindi cha miaka mitano, na kutoa ruzuku mbali mbalikwa tafiti zinazolenga kushughulika na magonjwa sugu na majanga.

ii. Itaongeza uwezo wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) katika rasilimali watu, miundombinu na teknolojia ili kuweza kufanya tafiti za kina kuhusu magonjwa, chanjo, dawa na tiba.

iii. Itajenga maabara kubwa na ya kimataifa itayotumika kwa utafiti katika ukanda wa kusini mwa Afrika.

iv. Itawezesha tiba asilia na kulinda hati miliki za wavumbuzi nchini kwa kuiwezesha

v. Bodi ya Tiba Asilia kufanya uthibitishaji, usajili na utafiti wa mimea, pamoja na sera ya kulinda haki miliki za wavumbuzi wa dawa nchini. Itaimarisha ushirikiano na sekta binafsi na taasisi zisizo za kiserikali katika sekta ya afya katika shughuli za utafiti na upatikanaji wa huduma za afya.

### 2.1.6. Dawa, Vitendea Kazi na Vitendanishi

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itajenga na kupanua viwanda vya dawa, chanjo na vifaa tiba, na itatoa ruzuku ya mitambo kwa wawekezaji wazawa, ili kuimarisha uzalishaji wa ndani na kupunguza utegemezi wa kuagiza dawa na vifaa nje ya nchi.

ii. Itaboresha uwezo wa Bohari Kuu na kuweka mfumo wa kufuatilia mahitaji na upatikanaji wa dawa na vitendea kazi ―stock levels‖ kwa muda halisi (real-time) na kuhakikisha kila zahanati, kituo cha afya na hospitali zinakuwa na dawa za kutosha na vitendea kazi wakati wote.

### 2.1.7. Mfumo Bora wa TEHAMA kwa Taarifa za Afya

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itaweka mfumo jumuishi wa TEHAMA kwa sekta ya afya nchi nzima ambao utawezesha ukusanyaji wa taarifa zote za afya kwa wakati halisi. Mfumo huu utasaidia kusaidia kupanga na kukadiria mahitaji halisi ya dawa, vifaa tiba, na rasilimali watu katika vituo vya afya; utaboresha ufuatiliaji wa huduma za kinga na matibabu kwa magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza, kurahisisha mawasiliano kati ya wahudumu wa afya na wagonjwa, na kukuza huduma za afya kwa njia ya simu (telemedicine) hususani maeneo ya vijijini. Aidha, mfumo huu utasaidia katika kuhifadhi taarifa za mgonjwa kwa usalama, kuongeza uwajibikaji, na kurahisisha uchambuzi wa takwimu kwa ajili ya kufanya maamuzi bora ya kisera.

# 2.2. KUTOA ELIMU BORA, BURE KWA WOTE



Elimu kama nyenzo muhimu ya taifa bora tulitakalo inapaswa kutazamwa upya na kufanyiwa maboresho makubwa. ACT Wazalendo inataka kuzalisha wataalamu katika fani na ujuzi mbalimbali unaoendana na wakati na kusaidia jamii ya Watanzania. Serikali ya ACT Wazalendo, itatoa elimu bora bila malipo (bure) katika shule za awali, msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, mpaka shahada ya kwanza, vyuo vya ufundi (VETA) na vyuo vya utabibu. Katika kufikia shabaha hiyo itafanya yafuatayo:

### 2.2.1. Elimu Msingi

i. Itapiga marufuku michango yote na kugharamia mahitaji ya msingi ya elimu, ikiwemo mitihani, masomo ya ziada, vitabu, chakula, ulinzi na miundombinu yote katika shule na vyuo vya serikali.

ii. Itaajiri waalimu wapya 325,000 (ikiwa ni walimu elfu 65 kila mwaka), ili kumaliza kabisa tatizo la uhaba wa walimu; na kuwajengea uwezo waalimu wote ili kuendana na mahitaji ya sasa.

iii. Itaongeza viwango vya mishahara ya walimu kwa asilimia ishirini (20%), pamoja na kupandisha madaraja kwa wakati na kutoa posho ya mazingira magumu kwa walimu wanaofanya kazi maeneo ya pembezoni.

iv. Itajenga na kuboresha maktaba na maabara za kisasa katika kila shule za sekondari na vyuo vya umma.

v. Itaajiri wafanyakazi wasio walimu, kama wataalamu wa mahabara, wakutubi, wanasaikolojia na walezi, ili kuhakikisha upatikanaji wa elimu na ubora wa malezi wakiwa shuleni.

vi. Itajenga na kuanzisha maktaba za kijamii (community libraries) katika kila kata, ili kukuza maarifa, ujuzi na kuendeleza utamaduni wa kujifunza.

vii. Itajenga vyumba vipya vya madarasa elfu ishirini na nane (28,000) kila mwaka, katika shule za msingi.

viii. Itajenga shule za sekondari ya juu (Advanced level) 250 ili kupanua wigo wa wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu.

ix. Itaimarisha na kuhamasisha mafunzo ya lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kigeni kama Kiarabu, Kichina, Kifaransa, Kirusi, Kihispania, Kireno, Kijerumani n.k.

x. Itarasmisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia kuanzia ngazi ya msingi hadi chuo kikuu.

xi. Itajenga nyumba za walimu laki moja (20,000 kila mwaka) ili kuweka mazingira mazuri kwa walimu vijijini na maeneo ya pembezoni.

xii. Itagawa bure vitaulo vya kujistiri kwa wasichana (pedi) ili kuweka mazingira mazuri na salama kwa wanafunzi wa kike.

xiii. Itasimamia utekelezaji na haki ya wasichana waliopata ujauzito, kabla ya kumaliza masomo, kuendelea na masomo yao na kutoa elimu rika.

xiv. Itaboresha mfumo wa udhibiti ubora wa elimu kwa kuongeza bajeti ya ukaguzi ili kutoa uhuru na kuimarisha utendaji wa kitengo cha udhibiti ubora wa elimu nchini.

xv. Itatokomeza kabisa hali watu kutokujua kusoma na kuandika kwa kupanua elimu ya watu wazima na kufanya programu mbalimbali za kujifunza kusoma na kuandika kwa Kiswahili na kwa lugha za kigeni, hususani kiingereza, kwa kushirikiana na asasi za kiraia, ikiwemo taasisi za dini, na sekta binafsi.

xvi. Itaboresha mfumo wa mafunzo kwa vitendo kwa walimu kwa kuongeza muda wa mafunzo kwa vitendo kuwa wa mwaka mmoja wenye malipo.

### 2.2.2. Elimu ya Juu

i. Itaweka huduma ya intaneti bure, bora na ya uhakika katika shule za sekondari na vyuo vyote vya umma mpaka ngazi ya shahada ya kwanza.

ii. Itajenga vyuo vikuu vya umma vipya sita (6) vyenye uwezo wa kudahili wanafunzi wasiopungua elfu ishirini (20,000) kila kimoja katika mkoa wa Lindi, Kigoma,Simiyu, Tanga na viwili kwa upande wa Zanzibar – Unguja na Pemba.

iii. Itasamehe na kufuta madeni ya mikopo ya elimu ya juu iliyotolewa kwa wahitimu wa elimu ya juu.

iv. Itabadili sheria ya bodi ya mikopo ya elimu ya juu kuhakikisha mikopo ya elimu ya juu inatolewa kwa wanavyuo wote kwa ajili ya kujikimu (meals and accommodation).

v. Itavihakikishia vyuo vikuu uhuru na mamlaka kamili ya kuajiri na kusimamia maendeleo ya wafanyakazi wao katika vyuo.

vi. Itaajiri wahadhiri wasiopungua elfu tano (5000) ili kupunguza uwiano mkubwa uliopo kati ya wahadhiri na wanafunzi.

vii. Itadhibiti ubora wa elimu katika vyuo binafsi ili kuhakikisha kila chuo kinaandaa wahitimu walio bora.

viii. Itahakikisha fani zote zinapitia mafunzo kwa vitendo, yenye malipo, kwa kipindi kisicho pungua miezi sita.

ix. Itahakikisha ulinzi wa wanafunzi wa kike dhidi ya rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia.

x. Itajenga na kuboresha hosteli za kutosha kwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

xi. Itaweka mkakati maalum wa kuanzisha na kuboresha programu za mashirikiano na vyuo na taasisi za nje, kwa ajili ya kuwezesha wanafunzi, wahitimu na walimu kupata nafasi za mafunzo kwa vitendo nje ya nchi (Extended and International Practical Learning Strategy), ili kubadilishana ujuzi na uzoefu kimataifa.

### 2.2.3. Elimu ya Ufundi

i. Itatoa elimu ya mafunzo ya ufundi (VETA) bure.

ii. Itajenga na kuimarisha vyuo vya ufundi stadi katika kila halmashauri ya wilaya, kambi za JKT na magereza.

# 2.3. MAJI SAFI NA SALAMA KWA WOTE



Ili kuhakikisha upatikaji wa maji safi na salama kwa kila Mtanzania, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itahakikisha upatikanaji wa maji ya bomba kwa ngazi ya kaya, ndani ya miaka mitano, kwa utaratibu na gharama nafuu.

ii. Itawekeza kiasi cha shilingi Trilioni 10 ndani ya miaka mitano, wastani wa shilingi Trilioni 2 kwa kila mwaka, kwenye kumaliza kabisa tatizo la maji safi na salama kwa wananchi. Hii ni pamoja na kujenga na kupanua miundombinu ya maji safi na maji taka.

iii. Itatoa ruzuku kwa mamlaka za maji ili kuziwezesha kupanua na kuboresha miundombinu ya maji katika maeneo yao. Upanuzi wa miundombinu ya maji utazingatia mahitaji, usawa na mipango ya miji/ vijiji.

iv. Itatoa maji bure kwa kaya masikini, na watu wenye ulemavu wanaoishi kwenye mazingira magumu.

v. Itawekeza katika teknolojia, ubunifu na uvumbuzi ili kuboresha upatikanaji, utunzaji, usambazaji na uvunaji wa maji ya mvua na udhibiti wa maji taka nchi nzima.

vi. Itatoa mikopo ya bei nafuu kwa ajili ya ujenzi wa visima vya maji, kama mpango wa muda mfupi na wa dharura, kwa jamii zenye changamoto kubwa ya maji.

vii. Itafanya maboresho makubwa ya miundombinu chakavu ya maji mara kwa mara ili kupunguza upotevu wa maji kwenye miji, manispaa na vijiji.

viii. Itatengeneza miundombinu ya majitaka na kuunganisha majumbani katika miji na majiji.

## 2.4. NISHATI



Tanzania imejaaliwa utajiri mkubwa wa nishati ya gesi asilia, vyanzo vya maji vinavyotumika kuzalisha nishati na vyanzo vingine. Hata hivyo, bado utajiri huo haujatumika kikamilifu katika kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa umeme kwa Watanzania wengi. Licha ya utajiri huu mkubwa wa nishati, bado vyombo vya usafiri vinategemea kwa kiasi kikubwa mafuta kutoka nje.

ACT Wazalendo inataka kila nyumba iwake taa; magari yatumie gesi asilia kama nishati mbadala wa mafuta; na nishati ya gesi itumike kikamilifu kupikia. Ili kufikia lengo hilo, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itaongeza kiasi cha umeme kinachozalishwa kutoka megawati 4,031 za sasa mpaka megawati 9,365 kufikia mwaka 2030. Kati ya hizo, megawati 3,716 zitatokana na umeme unaozalishwa na maporomoko ya maji (hydroelectric power plants), megawati 5,017 zitazalishwa kutoka gesi asilia, megawati 512 zitazalishwa kutokana na vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu ikijumuisha umeme jua, upepo na joto ardhi na megawati 120 kwa makaa ya mawe.

ii. Itashusha bei ya kununua umeme kwa uniti kwa asilimia 50 na kuhakikisha umeme unapatikana nyumba kwa nyumba.

iii. Itapunguza gharama ya kuunganisha umeme kwa matumizi ya nyumbani hadi kufikia shilingi elfu ishirini na tano tu (25,000), mijini na vijijini.

iv. Itahakikisha uunganishaji wa umeme ndani ya siku 10, baada ya kufanya malipo.

Itaboresha miundombinu ya kusafirisha umeme ili kupunguza upotevu wa umeme hadi kufikia chini ya asilimia 10 na kuimarisha usambazaji wa uhakika mijini na vijijini.

v. Itasambaza bomba la gesi majumbani kwa matumizi ya kupikia ili kupunguza gharama za sasa za matumizi ya mitungi ya gesi na kuokoa mamilioni ya misitu inayopotea.

vi. Itaziunganisha kaya masikini na huduma ya umeme bila malipo kupitia mfumo wa hifadhi jamii.

vii. Itaongeza matumizi ya gesi asilia (CNG) kwenye magari, kwa kuunganisha magari yote ya serikali, mabasi ya mwendokasi, malori, mabasi ya mikoani na vyombo vyengine.

viii. Itahakikisha ujenzi wa vituo vikubwa vya gesi asilia (CNG) katika mikoa yote ya Tanzania.

ix. Itaimarisha na kuongeza uwezo wa wazawa kuwekeza kwenye ujenzi wa vituo vya gesi asilia ili kuhakikisha upatikanaji wa gesi nchini kote.

# 2.5. HIFADHI YA JAMII KWA WOTE



Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itawezesha kila Mtanzania kujiunga na Mfumo wa Hifadhi ya Jamii utakaomuwezesha kupata bima ya afya, bima ya majanga na ajali, pensheni na kupata mkopo nafuu.

ii. Itapunguza michango kwa wafanyakazi wa sekta rasmi kwenye hifadhi ya jamii kutoka asilimia ishirini (20%), ya sasa, mpaka asilimia kumi na tano (15%).

iii. Itawaunganisha na kuchangia elfu kumi (10,000) kwa kila elfu thelathini (30,000) kwa Watanzania walio katika sekta isiyo rasmi – wakulima, wavuvi, wafugaji, madereva, makuli, bodaboda , mama lishe, mama mboga n.k.

iv. Itawaunganisha na kuchangia asilimia 100 ya kila mwananchi masikini aliye kwenye mpango wa kaya masikini.

v. Itatumia Hifadhi ya Jamii kama nyenzo ya kukuza uwekaji akiba nchini ili kuwa na vyanzo vya mitaji ya uwekezaji wa ndani katika sekta za kilimo, umwagiliaji na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao.

vi. Itatoa pensheni kwa kila Mtanzania aliye katika mfuko wa hifadhi ya jamii na aliyefikisha umri kuanzia miaka 60.

vii. Itatunga sheria kuwezesha mifuko ya hifadhi ya jamii kutoa mafao ya bima ya afya, bima ya mazao na majanga (crop Insurance) kwa shughuli za kilimo na mifugo na fao la bei (price stabilization benefit).

viii. Itadhibiti matumizi mabaya ya fedha za mifuko ya hifadhi ya jamii na kuwa na miradi yenye tija kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

ix. Italipa madeni yote inayodaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa mkupuo ili kuiwezesha mifuko kujiendesha na kuhudumia wanachama wake kwa wakati.

x. Itafanya maboresho ya sheria ya fedha za halmashauri na kutenga fedha ya asilimia 10 iliyopaswa kwenda kwenye makundi maalum ielekezwe kwenye mfumo wa hifadhi ya jamii na mikopo itolewe na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa wanachama.

# 2.6. HUDUMA BORA ZA MAWASILIANO NA UHURU WA HABARI



Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itapunguza gharama na kuondoa ukomo wa vifurushi (bundles) vya mawasiliano.

ii. Itafuta sheria zote kandamizi na zinazopora uhuru wa habari, wanahabari na vyombo vya habari; na kutunga sheria mpya zinazotoa uhuru wa habari na zitakazowezesha uhuru wa wanahabari na vyombo vya habari.

iii. Italinda na kuboresha maslahi na hali za waandishi wa habari kwa kuhakikisha vyombo vya habari vinawapa wanahabari mikataba ya ajira na malipo mazuri.

iv. Itahakikisha upatikanaji wa mtandao wa intaneti bure, bora na wenye kasi katika taasisi zote za umma na maeneo ya wazi.

v. Itahakikisha upatikanaji wa uhakika wa huduma za mawasiliano ya simu, intaneti, radio na televisheni nchi nzima, kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya mawasiliano mijini na vijijini.

vi. Itasimamia na kuboresha mifumo ya ulinzi wa taarifa na faragha katika mawasiliano na matumizi ya mtandao.

vii. Itakabiliana na kudhibiti utapeli na wizi wa mtandao kwa kuvijengea uwezo wa kitaalam vitengo vya ulinzi na kuchukua hatua kali dhidi ya wahalifu wa kimtandao.

viii. Itadhibiti ubora na kupunguza kodi za uingizaji wa simu janja na kompyuta ili kuhakikisha wananchi wanapata vifaa bora vya mawasiliano kwa bei nafuu.

ix. Itahakikisha mabaraza ya madiwani na bunge linarusha mubashara vikao vyake vyote kwa kutumia mitandao ya kijamii na vyombo vyengine vya habari.

x. Italiboresha na kulijengea uwezo wa kifedha, kiteknolojia, kiutendaji na wa miundombinu Shirika la TTCL, ilikuweza kushindana na mashirika mengine ya mawasiliano, ndani na nje ya nchi.

xi. Itahakikisha vyombo vya habari vya serikali vinatumika kikamilifu katika kuibua sauti, mijadala na hisia za kweli za wananchi pasipo ubaguzi wa aina yeyote.

xii. Itatoa ruzuku na motisha kwa vyombo vya habari, wanahabari na Watanzania wanaoan daa programu mbalimbali za kijamii zinazoeleza kuhusu historia, utamaduni, uchumi, maendeleo ya kisayansi na hali ya kisiasa kwa ajili ya kujenga maarifa na kutoa taarifa kuhusu Tanzania na bara la Afrika, ndani na njeya nchi.

# 3. KUBORESHA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA UCHUKUZI



Serikali ya ACT Wazalendo itatumia nafasi ya Tanzania kijiografia, ya kuzungukwa na nchi nyingizisizo na bahari, kufaidika kiuchumi na kuhudumia nchi nyingine. Shabaha kuu ni kuifanya

Tanzania kuwa kituo kikuu cha usafirishaji wa majini (Maritime Hub) katika bara la Afrika na kituo kikuu cha biashara (Trade & Logistics Hub) katika eneo la maziwa makuu, kwa njia za bandari, reli, barabara na anga. Zaidi, serikali itatengeneza na kutekeleza sera sahihi zitakazohakikisha Watanzania wananufaika kwa kufanya biashara na nchi zote zinazotuzunguka kwa kuondoa urasimu katika kupeleka bidhaa nje ili kuongeza mapato yao na fedha za kigeni.

Aidha, serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha barabara zote zinapitika wakati wote ili kusaidia wazalishaji wa ndani na kurahisisha usafiri wa abiria na mizigo, kuondoa kabisa foleni na kuharakisha usafiri na usafirishaji kuwa nafuu zaidi. Barabara zote za taifa na mikoa zitakua za kiwango cha lami na kuondoa kabisa barabara za vumbi Tanzania ndani ya miaka mitano.

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itaharakisha ujenzi wa reli ya kati hadi Mwanza na kuanza ujenzi mpya wa kipande cha Tabora – Kigoma – Mpakani mwa Burundi; na kufufua reli ya Kaskazini, kutoka Dar – Tanga – Arusha.

ii. Itajenga reli ya kisasa [SGR] ya Kusini Dar – Lindi – Mtwara – Ruvuma, kwa ajili ya kusafirisha abiria na mizigo.

iii. Itajenga reli kuunganisha maeneo ya migodi ya Mchuchuma – Liganga na Kabanga Nickel hadi bandari za Mtwara, Dar es Salaam na Bagamoyo.

iv. Itajenga na kuhamasisha matumizi ya usafiri wa reli za mijini katika majiji ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

v. Itahakikisha reli ya kisasa ya SGR inatumika kikamilifu kusafirisha mizigo, ili kupunguza msongamano, uharibifu wa barabara na gharama za usafirishaji.

vi. Itaongeza treni na kuongeza safari, kwa kutoa huduma ya usafiri wa treni kwa saa 24 kwa siku.

vii. Itawezesha ujenzi wa barabara ya korosho (Cashew Ring Road) ya Nangurukuru – Liwale – Nachingwea – Masasi – Newala – Tandahimba – Mtwara kutokana na mapato ya ushuru wa korosho.

viii. Itanunua vivuko vikubwa vipya 15 na kukarabati vilivyopo ili kutoa huduma bora za usafiri za uhakika, haraka na nafuu.

ix. Itaiwezesha TEMESA kusimamia, kukarabati na kuendesha vivuko vyote nchini.

x. Itapandisha barabara zote za wilaya kuwa kiwango cha changarawe au lami; na itahakikisha barabara zote za mikoa na barabara kuu zinakuwa za lami.

xi. Itatenga na kuzifikisha katika utendaji fedha za kuanzisha miradi mipya na kukarabati barabara chakavu.

xii. Italivunja shirika la ndege la ATCL na kuanzisha shirika jipya la ndege litakalo miliki na kununua ndege na kuondokana na utaratibu wa sasa wa TGFA kumilikindege.

xiii. Itamarisha mifumo ya usimamizi wa shirika la ndege na kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege ili kutoa huduma bora na zenye ufanisi.

xiv. Itakuza ushirikiano wa sekta binafsi na serikali katika usafiri wa baharini ili kuboresha upatikanaji wa huduma bora, haraka na za bei nafuu kwa watumiaji.

xv. Itapitia mikataba na makubaliano ili kukwamua uendelezaji wa eneo maalum la kiuchumi la Bagamoyo kwa maslahi ya taifa.

xvi. Itaimarisha Bandari ya Mtwara ili kuhudumia Ushoroba wa Mtwara (Mtwara Corridor) na kutumika kusafirisha mizigo kwenda nchi jirani za Malawi, Msumbiji na Zambia; na kuifanya Mtwara kuwa kituo cha huduma kwa miradi ya uwekezaji wa mafuta na gesi, kusini mwa Tanzania na Kaskazini mwa Msumbiji.

xvii. Itaimarisha Bandari ya Tanga na kukamilisha uwekezaji wa Bandari ya Mwambani, na kuifanya Tanga kuwa kitovu cha usafirishaji kwa Ukanda wa Kaskazini mwa Tanzania.

xviii. Itaiongezea uwezo Bandari ya Kigoma ili kuweza kuhudumia mizigo inayotoka na kwenda mashariki ya Kongo pamoja na nchi ya Burundi.

xix. Italiboresha na kulijengea uwezo wa kifedha, kiteknolojia na kiutendaji Shirika la Posta ili lishiriki kikamilifu na kiushindani katika biashara mtandao (e-commerce) kwa kujenga maghala makubwa sita (warehouse), katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Tanga na Mtwara, kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi.

xx. Italiwezesha Shirika la Posta kuanzisha ghala maalum nchini China, Uturuki, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ili kuwezesha usafirishaji wa bidhaa kwenda na kutoka nchi hizo.

xxi. Italiwezesha Shirika la Posta kusimamia kwa ukamilifu mfumo wa anuwani ya makazi na kuweka mfumo jumuishi wa kiteknolojia utakaowezesha usafirishaji salama na rafiki wa bidhaa za wafanyabiashara, watoa huduma mbalimbali na watu kutuma na kupokea mizigo ndani na nje ya nchi.

xxii. Italifungamanisha Shirika la Posta na miundombinu mikuu iliyopo nchini, ikiwemo bandari, reli ya kisasa ya SGR na viwanja vya ndege; na kuhakikisha kwamba taasisi zote za kiserikali zinalitumia Shirika la Posta kwa ajili ya kutuma na kupokea mizigo ndani na nje ya nchi.

# 4. KUSIMAMIA HAKI, USAWA, DEMOKRASIA NA USALAMA WA RAIA



Serikali ya ACT Wazalendo inaamini katika mifumo ya Demorasia Shirikishi inayozingatia misingi ya haki, uwazi, usawa na uwajibikaji. Inatambua kuwa Tanzania itaendelea kuwa kisiwa cha amani na ustawi endapo tu haki za kijamii na haki za watu zitaheshimiwa. Shabaha yetu kubwa zaidi ni kuifanya Tanzania kuwa sehemu salama zaidi duniani kwa kuhakikisha inakua na katiba mpya, iliyo bora inayotokana na wananchi; na inakuwa na mfumo thabiti wa haki jinai na haki jamii, inayoongozwa na misingi ya demokrasia na usawa wa kijamii.

Serikali ya ACT Wazalendo itajenga taifa lenye haki, usawa na demokrasia ya wote, kwa maslahi ya wote; haitafumbia macho wala kusahau madhila ya utekaji, kupotea kwa raia, kukithiri kwa vitendo rushwa, ufisadi na ubadhirifu. Itasimamia misingi ya haki katika nyanja zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

# 4.1. KATIBA MPYA



Serikali itakayoongozwa na ACT Wazalendo, ndani ya mwaka mmoja, itafufua na kukamilisha mchakato wa kuandika Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwashirikisha Watanzania kikamilifu.

Pamoja na mambo mengine, serikali ya ACT Wazalendo itasimamia mambo yafuatayo katika uandikaji wa Katiba Mpya:

i. Itaivunja Tume ya Uchaguzi iliyopo ndani ya siku 200 na kuanzisha Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (iliyo huru kweli), ambayo mchakato wa upatikanaji wa watumishi wake wote utakuwa kwa mfumo na utaratibu wa uwazi, haki na huru; na itahakikisha watumishi hao, kwa namna yeyote ile, hawatawajibika kwa Rais, wala viongozi wowote wa kisiasa na kiserikali, nje ya Tume.

ii. Itapunguza madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

iii. Itaboresha muundo wa Muungano ili kuwa na Muungano wa Usawa, Haki na wenye Kuheshimiana, na kusimamia uundwaji wa muundo wa serikali tatu.

iv. Itaimarisha uhuru na uimara wa mihimili yote ya dola na kuhakikisha mgawanyo wa kweli, katika matendo na kimantiki, kati ya mihimili ya Bunge, Serikali na Mahakama.
v. Itasimamia uwepo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa' badala ya kulimbikiza viongozi wa chama kimoja.

vi. Italeta mfumo bora wa kuendesha Serikali hasa za mitaa – kwa kuwezesha ugatuaji (madaraka zaidi ya kiusimamizi, kiutendaji na kimaamu yatawekwa kwa Serikali za Mitaa badala ya Serikali Kuu).

vii. Itawafuta wakuu wa wilaya na kuweka utaratibu wa wananchi kuwa na haki na wajibu wa kuchagua, kuwasimamia na kuwawajibisha wakuu wa mikoa.

viii. Itajali maslahi mapana ya Taifa letu na kuimarisha uwajibikaji, kwa kurejesha mamlaka ya maamuzi kwa wananchi.

## 4.2. KUPAMBANA NA RUSHWA NA UFISADI



Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itachukua hatua kali dhidi ya watu na taasisi zote zilizohusika na zinazohusika na vitendo vya rushwa, ufisadi na ubadhirifu kutokana na ripoti mbali mbali za kiserikali, ikiwemo ripoti ya Mkaguzi wa Serikali (CAG).

ii. Itapiga marufuku mtu yeyote aliyepatikana na hatia ya rushwa na makosa ya kifedha kufanya kazi/ biashara na taasisi yeyote ya serikali.

iii. Itawafukuza uanachama, kuwafuta uongozi na kuwachukulia hatua nyingine kali za kisheria viongozi wa kuchaguliwa na watu wote watakaojihusisha na vitendo vya rushwa na ubadhirifu.

iv. Itapiga marufuku viongozi na watumishi wa serikali kupewa zabuni katika miradi ya serikali.

v. Itaandaa na kuchapisha orodha ya makampuni na taasisi zinazotoa rushwa kupata miradi, ili kuondoa mianya ya rushwa katika manunuzi hasa ya nje, kwa kushirikana na mataifa ya jirani na rafiki.

vi. Itaweka na kuusimamia utaratibu wa kisheria utakaohakikisha kwamba watu wote na makampuni yote yatakayopatikana na hatia ya kutoa au/ na kupokea rushwa mali zao zinataifishwa.

vii. Itaifanya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwa chombo huru na cha kitaalamu kisichofungamana na siasa katika utendaji wake.

viii. Itatekeleza kikamilifu sera ya serikali ya uwazi (Open Government Policy) na uhuru wa habari katika kuhakikisha uwajibikaji na kuzuia vitendo vya rushwa, ufisadi na ubadhirifu.

ix. Itaboresha sheria ya kuwalinda watoa taarifa (Whistle Blowers Act).

## 4.3. KUREKEBISHA MFUMO WA SHERIA NA UPATIKANAJI HAKI



Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itaanzisha Ofisi ya Uwakili wa Umma (Office of the People's Attorney), itakayokuwa huru na yenye kujitegemea, itakayohakikisha kila mwananchi anapatiwa haki ya uwakilishi kwenye masuala na mienendo ya kesi mbele ya sheria katika ngazi zote za utoaji haki (hususani masuala ya jinai); na itakayokuwa na jukumu la kusimamia na kulinda haki za wananchi.

ii. Itatathmini na kuboresha sheria za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kuondoa ushiriki wa Wakuu wa Wilaya na kuhakikisha wananchi washiriki kikamilifu katika kuzisimamia serikali za mikoa na mitaa.

iii. Itaboresha mazingira ya kufanyia kazi, makazi, na malipo ya watumishi wa vyombo vyote vya kutoa na kusimamia haki nchini.

iv. Itahakikisha Serikali inatii na kutekeleza hukumu na maagizo ya mahakama dhidi ya serikali ndani ya siku 90.

v. Itaimarisha na kulinda uhuru wa mihimili mitatu ya dola ili kuhakikisha kuwa inatimiza wajibu wake kwa mujibu wa sheria na Katiba ya nchi yetu.

vi. Itahakikisha mfumo wote wa utoaji haki unakuwa na unaendeshwa kwa lugha ya Kiswahili, ikiwemo utunzi na utafsiri wa sheria zote na uendeshaji wa mashauri.

vii. Itahakikisha masuala yote yanayohusu maslahi ya umma yanawekewa utaratibu wa uwazi na rafiki (ikiwemo wa kimtandao) kuwezesha kuufikia umma mpana.

viii. Itaandaa utaratibu maalum na rasmi wa kufanya tathmini kuu na shirikishi ya mfumo wa sheria na upatikanaji haki, kila baada ya miaka miwili, utakaoongozwa na Chama cha Mawakili wa Tanganyika na Zanzibar, kwa kushirikiana na Bunge, Mahakama, Chama cha Mawakili wa Serikali, Ofisi ya Uwakili wa Umma, Taasisi za Kiserikali, Waandishi wa Habari, Wanataaluma, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, Wadau wa Haki na Wananchi kwa Ujumla.

# 4.4. KUHAKIKISHA ULINZI NA USALAMA WA RAIA



ACT Wazalendo tumedhamiria kuhakikisha Tanzania inakuwa sehemu salama kwa wananchi kufanya shughuli zao, kuishi na kupiga hatua za maendeleo bila hofu, wasiwasi na mashaka. Katika kulifanikisha hili, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itafanya uchunguzi huru na wa kitaalam wa matukio yote ya utekaji, utesaji, upoteaji na mauaji ya raia na kutoa ripoti ya kina kwa umma na kuchukua hatua dhidi ya wote wanaohusika ndani ya siku 100.

ii. Itatoa msaada wa kisaikolojia, kijamii na kiuchumi kwa watu na jamii zilizoathiriwa na vitendo vya ukiukwaji haki.

iii. Italiunda upya Jeshi la Polisi na kuliimarisha kitaaluma, kwa kulitoa kuwa chombo cha ‗mabavu' (police force) na kulifanya kuwa chombo cha huduma (police service).

i. Itakomesha vitendo vya utekaji, utesaji, uonevu, ubaguzi wa kiitikadi, unyanyasaji, uvunjifu wa haki za binadamu na mauaji ya raia na kuvunja magenge yote ya uhalifu na kuwachukulia hatua kali watu wote wanaohusika na vitendo hivyo.

ii. Itaipa uwezo wa kibajeti, kiweledi na kisheria Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Ofisi ya Uwakili wa Umma, ili kusimamia vyombo vya dola kulinda haki na usalama wa watu na mali zao kwa uhuru.

iii. Itafanya mapitio ya Sheria ya Usalama wa Taifa na kuwaondolea mamlaka waliyopewa ya kukamata na kuwashikilia watu bila kuchukua hatua za sheria (arbitrary detention).

iv. Itafanya marekebisho ya sheria ya ugaidi na sheria nyingine kandamizi zinazotumika kiholela kwa ajili ya kupora haki za wananchi.

v. Itatunga sera ya mfumo wa Haki za Kijinai [Criminal Justice Policy] ili kuimarisha mifumo ya kitaasisi na kiuendeshaji wa taasisi za usimamizi wa jinai.

vi. Itaboresha mfumo wa upelelezi wa mashauri kwa kusimamia na kuweka ukomo wa muda wa upelelezi kwa makosa yote ili kupunguza mrundikano wa kesi.

vii. Itatunga sheria moja ya dhamana (Bail Act) kwa makosa yote ya jinai na kuweka utaratibu wa dhamana kwa makosa yote.

viii. Itaimarisha utaratibu wa upatikanaji taarifa, uchunguzi na doria kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama ili kudhibiti matukio ya uhalifu na mauaji mijini na vijijini.

# 4.5. KUBORESHA MASLAHI NA UTENDAJI WA WATUMISHI WA UMMA



Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itaweka utaratibu wa kisheria utakaoelekeza uteuzi wa Viongozi wa Tume ya Maadili ya Umma kufanywa na Tume ya Kijaji, chini ya Jaji Mkuu na kufanyiwa usaili na kuthibitishwa na Bunge, ili kuhakikisha wanawajibika kwa wananchi.

ii. Itaunda Kamisheni ya Maadili ya Jeshi la Polisi ili kusimamia weledi na maslahi ya polisi hasa katika kuhakikisha jeshi la polisi halitumiki kisiasa.

iii. Itapambana na unyanyasaji wa kijinsia makazini ili kutengeneza mazingira salama ya kazi, hasa kwa wanawake, na kuhakikisha Tanzania inaridhia na kusimamia utekelezaji wa mapatano ya shirika la kazi duniani (ILO, C190) yanayoelekeza kuondoa ukatili sehemu za kazi.

iv. Itafanya malipo yote ya madeni ya posho, mishahara na stahiki za nyuma za wafanyakazi ndani ya mwaka mmoja na itahakikisha fedha zote za wafanyakazi zinalipwa kwa wakati.

# 4.6. WANAWAKE, WAZEE NA WATU WENYE ULEMAVU



Serikali ya ACT Wazalendo inataka kuongeza ushiriki wa wanawake katika shughuli za maendeleo na uongozi; na kuhakikisha heshima ya wazee inalindwa na kutunzwa; pamoja na watu wenye ulemavu wanapata nafasi ya kushiriki shughuli za maendeleo na kufaidika na maendeleo ya taifa. Hakuna mtu atakaeachwa nyuma katika serikali tutakayoijenga, kwa kuwa tunamaanisha tunaposema tunajenga Taifa la Wote kwa Maslahi ya Wote.

### 4.6.1. Kuongeza Ushiriki wa Wanawake katika Uongozi na Maendeleo

Serikali ya ACT – Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itahakikisha uwiano wa ushiriki wa 50 kwa 50, kwa wanawake na wanaume, katika ngazi zote za uongozi kwenye nafasi za kuteuliwa, kwa kuzingatia misingi ya uwezo, weledi na kitaalamu.

ii. Itatunga sera na sheria zitakazohakikisha angalau asilimia 30 ya manunuzi na huduma zote za ndani zinazofanywa na serikali kuu na serikali za mitaa zitatokana na biashara zinazomilikiwa na zinazoendeshwa na wanawake.

iii. Itaondoa kodi na kuwezesha upatikanaji bure wa bidhaa za taulo za kike katika shule za msingi na sekondari Tanzania nzima.

iv. Itadhibiti mimba za utotoni kwa kuweka mazingira salama na kutoa elimu rika katika jamii ili kukabiliana na ukatili na unyanyasaji wa kingono.

v. Itasimamia haki ya kupata elimu kwa wahanga wa mimba za utotoni, kwa kuhakikisha kila mtoto wa kike aliyepata mimba akiwa shule anamaliza elimu yake kama ilivyokusudiwa.

vi. Itakomesha ukatili dhidi ya wanawake na watoto, hasa ukatili wa kingono, kimwili na udhalilishaji wa kimtandao kwa kuongeza maafisa ustawi wa jamii katika kila kijiji na mtaa na kujengea uwezo na kuimarisha kitengo cha dawati la kijinsia kidijitali.

vii. Itarekebisha na kuboresha mifumo ya uwakilishi wa wanawake katika bunge na halmashauri (viti maalumu), ili kukuza ushiriki na uwakilishi wa wanawake katika vyombo hivyo.

### 4.6.2. Kuwatunza na Kuwaenzi Wazee

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itahakikisha kila mzee anapata pensheni kupitia mfumo wa hifadhi ya jamii, kwa wakati na bila bugudha.

ii. Itatokomeza ukatili, utapeli na unyanyasaji dhidi ya wazee kwa kuwachukulia hatua kali za kisheria watu wote wanaojihusisha na vitendo hivyo.

iii. Itatoa kipaumbele na msisitizo katika upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii kwa wazee wenye mahitaji.

### 4.6.3. Kushirikisha Watu wenye Ulemavu

Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itatenga na kuhakikisha angalau asilimia 5 ya ajira zinazozalishwa zinapatikana kwa watu wenye ulemavu.

ii. Itaziwezesha kaya maskini zinazolea watoto na watu wenye ulemavu kwa kuzipatia mahitaji muhimu.

iii. Itahakikisha kupatikana taarifa muhimu kwa watu wenye ulemavu kwa kuwezesha utafsiri kwa lugha ya alama na nukta nundu.

iv. Itasimamia utekelezaji wa sheria inayowawezesha watu wenye ulemavu kutumia miundombinu na ofisi za umma kwa urahisi na usalama zaidi.

v. Itahakikisha upatikanaji wa uwakilishi wa haki na wenye tija wa watu wenye ulemavu katika uongozi, ngazi za maamuzi na shughuli za kuingiza kipato.

vi. Itakomesha dhulma, unyanyasaji na ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu.

# 5. KULINDA NA KUSIMAMIA ARDHI NA RASILIMALI ZA TAIFA



Tanzania ni nchi yenye neema kubwa sana. Rasilimali asili zilizopo nchini hazitoi taswira halisi ya hali zetu kama wananchi. Utajiri wa rasilimali zetu ulipaswa kutufanya tuogelee kwenye maisha ya staha na kheri; tuserebuke kwenye ukwasi; na tuwe mfano wa kuigwa kwa wenzetu barani Afrika na kwa Nchi za Kusini. Haijawa na haiko hivyo. Watanzania, badala yake, wameku wa na wamefanywa watu ―MAKANTA‖ – ―Masikini Katika Nchi Tajiri‖.

Ardhi zetu zinaporwa; mbuga na misitu yetu inauzwa; mito na maziwa inapigwa mnada; madini, mafuta na gesi yote yanafanywa milki ya genge la walafi wachache na inatumika kuwatajirisha wao na wageni – watu wa nchi za magharibi; wanyama wetu wanawindwa; bahari na visiwa vyetu vimebinafsishwa; leo na kesho yetu iko gizani; na, mustakabali wetu unachezewa. Hili halipaswi kuvumilika na kuendelea kuwa hivi. Serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha upatika naji na ulinzi wa ardhi na rasilimali zote za taifa, kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi wa sasa na vizazi vijavyo, kwa kutengeneza mifumo thabiti ya kunufaika na ukwasi wa rasilimali zilizopo. Itahakikisha wananchi wa Tanzania wanapata taarifa sahihi za mikataba ya rasilimali ambayo serikali zote zimewahi kuingia na mikataba yote itakayoingiwa itakuwa wazi kwa umma ili wananchi waweze kuamua kuhusu rasilimali zao.

# 5.1. UPATIKANAJI, MATUMIZI NA ULINZI WA ARDHI KWA WANANCHI



Kwa kutambua kwamba ardhi ni uhai na chanzo kikuu maisha ya staha na maendeleo ya watu na jamii kwa ujumla, serikali ya ACT Wazalendo imedhamiria kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha upatikanaji na ulinzi wa ardhi kwa wananchi wote Imedhamiria kurejesha nafasi ya wananchi katika usimamizi wa ardhi na kuhakikisham thamani ya ardhi inakuwa katika matumizi na shughuli za uzalishaji, badala ya ubidhaishaji na uhodhi na umiliki wa ardhi usio na tija. Kwa msingi huu, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itarejesha ardhi kwa wananchi walioporwa na kunyang‘anywa kutokana na ubinafsishwaji na uwekezaji holela uliofanywa na serikali zilizopita.

ii. Itarejesha ardhi za vijiji zilizochukuliwa na kuwekwa sehemu ya ardhi ya hifadhi na kisha kuitenga kwa wafugaji na wakulima, ili kumaliza kabisa migogoro kati ya jamii hizo.

iii. Itafuta na kurejesha ardhi zote za vijiji zilizotelekezwa na ambazo haziendelezwi; na kugawa ardhi kwa vijana na makundi yenye uhitaji vijijini, kwa ajili ya matumizi ya uzalishaji.

i. Itaunda Tume ya Taifa ya kuchunguzi, kupitia na kuchora upya mipaka ya ardhi yote, kwa kushirikiana kikamilifu na wananchi, ili kutenga na kugawa ardhi kwa wananchi kulingana na mahitaji ya sasa na baadae.

iii. Itahakikisha wananchi wanakuwa sehemu ya umiliki katika miradi na shughuli za uwekezaji katika ardhi (Land for Equity).

iv. Itapinga uhamishaji holela wa ardhi ya kijiji kwenda makundi mengine ya ardhi.

Itafuta gharama za upimaji wa viwanja nchi nzima, serikali itachukua jukumu lake la kupima, kupanga, kuhakiki na kutoa hati mijini na vijijini.

v.

Itaingiza suala la ardhi kuwa sehemu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kutoa ulinzi kwa ardhi.

vi. Itaweka udhibiti na ukomo katika kiwango cha umiliki wa ardhi nchini na kuhakikisha ardhi inayomilikiwa inaendelezwa.

vii. Itahakikisha wananchi hawaondolewi kwenye ardhi yao bila kushirikishwa na kulipwa fidia kamili na ya haki, kabla ya kuondolewa na kuhamishwa.

viii. Itachukua hatua kali dhidi ya viongozi na watumishi wote watakaojihusisha na uuzaji, ukodishaji, ugawaji wa ardhi bila kuwashirikisha wananchi vijijini. Itahakikisha vijiji na miji yote ina mpango wa matumizi bora ya ardhi unaotekelezwa kwa mujibu wa sheria na kuzingatia usawa wa kijinsia na mazingira.

ix. Itajenga uwezo wa serikali ya kijiji kutambua, kusimamia, kutumia na kutatua migogoro ya ardhi ya kijiji.

x. Itaifuta sera mpya ya ardhi na kukataa sheria na mipango yote inayowekwa kuwezesha umiliki wa ardhi kwa watu wasio wananchi.

xi. Itazilinda kisheria na kuzipa hadhi sawa haki za umiliki wa ardhi ya kimila kama ilivyo kwa hati zinazotolewa na serikali kuu.

xii. IItabatilisha zoezi lote, lililofanyika kwa miaka yote, la kuwaondoa watu wa jamii ya kimasai na jamii nyingine za kiasili, kutoka kwenye maeneo yao ya asili; na itaweka katazo rasmi la kuwaondoa watu wa jamii za kiasili. Vivyo hivyo,

xiii. itafanya tathmini itakayoongozwa na watu wa jamii ya kiasili, pamoja na Tume ya Kijaji na wadau wenye utaalamu wa masuala ya ardhi na jamii za kiasili, kubaini ukiukwaji wa haki za jamii hizo na kuweka utaratibu na mpango maalum na endelevu wa matumizi ya ardhi kwa jamii hizo.

# 5.2. MADINI, MAFUTA NA GESI



Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itabadili mfumo wa kutoa leseni za uchimbaji wa madini kwa kuweka sharti la kupata kibali kutoka kwa serikali ya kijiji kupitia mkutano mkuu wa kijiji, kabla ya Tume ya Madini kutoa leseni. (Free Prior Informed Consent).

ii. Itaharakisha utekelezaji wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga wilayani Ludewa, mkoani Njombe, na mradi wa Kabanga Nickel wilayani Ngara, mkoani Kagera, na kuhakikisha utekelezaji unaanza ndani ya mwaka mmoja.

iii. Itaweka na kutamka katika katiba kwamba maliasili zote za madini, mafuta na gesi asilia, zitakuwa ni mali wananchi na hivyo zinapaswa kusimamiwa kikamilifu na kwa wakati wote na wananchi.

iv. Itabadili mfumo wa umiliki na uchimbaji wa madini, kutoka mfumo wa sasa wa kutoa leseni na kukusanya kodi na mrahaba, kwenda mfumo wa ―Umiliki na Ukandarasi‖ – ambapo Mwekezaji anakuwa mkandarasi na umiliki unabaki kwa serikali na wananchi kwa asilimia 100.

v. Itapitia mikataba yote ya uwekezaji na uchimbaji wa madini nchini, na kutazama upya kodi, misamaha, tozo na ushuru ili kulinda maslahi ya wananchi.

vi. Itaweka mikataba yote ya madini wazi kwa wananchi, iliyoingiwa na itakayoingiwa kwa ajili ya kukuza na kuongeza uwazi na uwajibikaji. Na itachukua hatua kali dhidi watumishi wote waliohusika katika mikataba yote iliyoingiwa na inayoliingizia taifa hasara, kutokana na uzembe na ufisadi.

vii. Itawezesha Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) kufanya tafiti na kutumia taarifa za utafiti, ili kuwawezesha Watanzania kufanya uchimbaji wa uhakika.

viii. Itahakisha wananchi wanaokutwa au waliopitiwa na miradi wanapatiwa fidia stahiki, itakayoambatana na shughuli mbadala na makazi mapya, fidia ya uharibifuwa kimazingira pamoja na kuweka mpango malum ya ujirani mwema.

ix. Itaondoa kodi na tozo kandamizi kwa wachimbaji wadogo na kuweka vivutio vitakavyo saidia Watanzania wengi.

x. Itaanzisha na kuongeza viwanda vya uchenjuaji, usafishaji na ukataji wa madini hapa nchini ili kuongeza thamani ya madini yetu.

xi. Itatunga sheria ya wajibu wa kampuni kwa jamii (CSR) kwa kuweka asilimia tatu (3%) ya faida itakayokwenda moja kwa moja kwa kijiji chenye mradi.

xii. Itarekebisha sheria ili kuhakikisha asilimia 10 ya mgawanyo wa mapato ya madini (mrabaha) inaenda kwenye vijiji vinavyozunguka mgodi.

xiii. Itaongeza muda wa leseni kwa wachimbaji wadogo kufikia miaka kumi ili kuwawekea mazingira mazuri ya kupata mitaji kutoka kwenye taasisi ya fedha.

ii. Itapitia mikataba ya uwekezaji wa Mradi wa Gesi Asilia (LNG Plant) na kuharakisha utekelezaji wake ili kuongeza ajira, mapato ya ndani na akiba ya fedha za kigeni kuto kana na mauzo ya gesi asilia nje ya nchi.

iii. Itawekeza katika utafiti na ugunduzi wa mafuta na gesi asilia na kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji mkubwa wa mafuta na gesi kusini mwa Afrika.

# 5.3. MISITU, BAHARI NA UHIFADHI



Serikali ya ACT Wazalendo itahakikisha yafuatayo:

i. Itarekebisha sheria za uhifadhi zinazotoa mamlaka makubwa kwa maafisa wa uhifadhi dhidi ya wananchi, ili kukomesha ukatili na ukiukwaji wa haki zabinadamu.

ii. Itabadili hadhi na utendaji wa jeshi usu la uhifadhi wa wanyamapori na misitu, kutoka taswira ya kijeshi kwenda kuwa chombo cha wananchi.

iii. Itavunja mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro na kuunda kampuni yenye kumilikiwa kwa ubia kati ya wananchi wanaoishi ndani ya hifadhi ya Ngorongoro na serikali

iv. Italinda na kuendeleza mfumo wa uhifadhi wa kijamii kwa lengo la kulinda mamlaka ya wananchi katika kusimamia rasilimali asili za wanyamapori, misitu na ardhi ya wenyeji.

v. Itazuia kupanuliwa kwa hifadhi na kupitia upya mipaka ya hifadhi, vijiji na makazi.

v. Itakabiliana kikamilifu dhidi ya uvamizi na uharibifu wa wanyama pori kwenye mazao na makazi ya watu; ikiwemo kwa kusimamia uvunaji wa tembo na wanyama waharibifu, ili kulinda uhai na mali za watu.

vi. Itaongeza idadi ya maafisa wa wanyamapori katika kila kijiji kinachozungukwa na hifadhi na kutumia mbinu za kisasa kukabiliana na wanyama vamizi na waharibifu.

vii. Itaongeza fidia ya uharibifu wa mazao, makazi na madhara kwa binadamu yanayosaba bishwa na wanyama vamizi na waharibifu, kufikia kiwango cha chini cha shilingi milioni 2; na itahakikisha fidia inalipwa kamili, kwa haki na wakati.

viii. Itaboresha mfumo wa usimamizi shirikishi wa rasilimali za bahari kwa kushirikiana na jamii za wavuvi na wajasiriamali wa bahari, katika kulinda fukwe, mikoko, matumbawe na viumbe vya bahari.

ix. Itaweka na kutekeleza mikakati ya athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa jamii za Pwani, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kuta za kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

x. Itazuia uporaji, uuzaji na ubinafsishaji wa sehemu za bahari na visiwa.

xi. Itaweka mikataba yote ya uhifadhi, bahari na misitu wazi kwa wananchi, iliyoingiwa na itakayoingiwa kwa ajili ya kukuza na kuongeza uwazi na uwajibikaji. Na itachukua hatua kali dhidi watumishi wote waliohusika katika mikataba yote iliyoingiwa na inayoliingizia taifa hasara, kutokana na uzembe na ufisadi.

# 5.4. KUKUZA UTALII



Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatato:

Itabadili mfumo wa mtalii kulipa akiwa nje ya nchi [Package Safari] na kuhamasisha mfumo wa watalii kufanya malipo wakiwa ndani ya nchi [Back-Pack Safari], ili kuhakikisha fedha hizo zinanufaisha watu wengi zaidi nchini.

Itaunganisha sekta ya huduma za hoteli za kitalii na sekta za uzalishaji ili kuhakikisha zinatumia bidhaa za kilimo,uvuvi na mifugo zinazotoka ndani ya nchi kwa asilimia 90.

Itaweka mpango maalum wa kutumia sekta ya sanaa, michezo na utamaduni kimkakati kama nyenzo za kukuza utalii nchini.

Itahamasisha utalii vijijini na kuziwezesha halmashauri na vijiji kuweza kupokea na kuhudumia watalii.

Itajenga na kuboresha miundombinu ya maeneo ya utalii ili kuwezesha kufikika kwa urahisi na kwa usalama.

Itatumia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na wadau mbali mbali katika kutanga za na kuhamasisha utalii; na kuhakikisha idadi ya watalii inaongezeka kufika watu Milioni 10.

Itaweka mfumo rahisi wa kikodi katika sekta (simple and stable fiscal regime) kwa kuondoa msururu wa kodi na tozo mbalimbali kwenye utalii.

Itachochea ujenzi na uboreshaji wa mahoteli na maeneo ya vivutio kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Itatanua wigo wa utalii kwa kuwekeza kwenye miundombinu, matangazo, ujenzi wa h oteli na huduma za kijamii katika ukanda wa kusini, nyanda za juu kusini na maeneo mengine nchini.

Itazalisha ajira mpya milioni 2.5 katika sekta ya utalii, kwa kuweka mazingira rafiki ya utalii na kwa kuhamasisha utalii wa bahari, mikutano, elimu na matibabu.

Itasimamia haki na maslahi ya waongoza watalii, wahudumu na wafanyakazi wote katika sekta ya utalii.

Itafungamanisha sekta ya utalii, sanaa, utamaduni na michezo kwa kujenga viwanja vikubwa vya michezo na kuhamasisha ujenzi wa kumbi za burudani katika mikoa ya Mtwara, Mwanza, Mbeya, Tanga na Dodoma.

# 6. KUIMARISHA MUUNGANO NA MAHUSIANO YA KIMATAIFA



Serikali ya ACT Wazalendo inataka kuimarisha muungano; na kuhakikisha kuwa tunakuwa na Muungano wa Haki, Usawa na Kuheshimiana. Muungano utakaozifanya pande mbili za muungano kuwa na mamlaka kamili kwa mambo yasiyo ya muungano na kushirikiana katika kuamua mambo ya Muungano. Serikali ya ACT Wazalendo inatambua kuwa muungano huu, ni muungano wa nchi mbili huru, yaani Tanganyika na Zanzibar; na muungano huu ni ishara ya udugu na mshikamano, na ni tunu ya taifa, ambayo hata hivyo inapaswa kudumu kwa heshima na manufaa ya pande zote mbili.

Vivyo hivyo, serikali ya ACT Wazalendo inataka kuirejesha heshima, jina, ukuu na nafasi ya Tanzania katika kilele cha diplomasia barani Afrika na katika nchi za Ukanda wa Kusini. Itatumia historia kubwa ya viongozi na taifa letu katika kuiendeleza ajenda ya Umajumui wa Afrika, unaolenga kuwezesha mashirikiano na mahusiano bora baina na miongoni mwa Waafrika; na kuimarisha mshikamano na mashirikiano ya mataifa ya Afrika na Jumuiya Umoja wa Afrika, ili kuhakikisha kuijenga Tanzania na Afrika madhubuti kijamii, kiuchumi, kisiasa, kisayansi, kiteknolojia, kijeshi na kiutamaduni. Pamoja na hayo, itasimama na kusimamia misingi ya haki, usawa, uhuru, heshima na mshikamano kwa watu na mataifa yote ulimwenguni.

# 6.1. KUIMARISHA MUUNGANO



Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo;

i. ACT Wazalendo itafufua mchakato wa kuandaa katiba mpya ya muungano inayoendana na mahitaji ya wakati chini ya msingi wa haki, heshima na usawa kama nchi mbili huru zilizoungana kwa hiari zao, ili kuwa na muungano wa haki, uwazi na usawa kwa kusimamia muundo wa serikali tatu

ii. Itaanzisha Akaunti ya Pamoja ya Fedha za Muungano kama ilivoelekezwa na Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kulipa malimbikizo ya madeni ya Zanzibar.

iii. Itahakikisha pande zote, Zanzibar na Tanganyika, zinanufaika na zitanufaika na mamlaka yake, kwa mambo yasiyo ya muungano, ndani na nje ya nchi.

# 6.2. UMOJA WA AFRIKA NA UHUSIANO WA KIMATAIFA



Serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itapitia mikataba yote ya kimataifa ya kiuchumi haswa inayohusu madini, mafuta, gesi, rasilimali za bahari, ardhi na mikopo ili kutazama maslahi ya taifa.

ii. Itasimamia kikamilifu Makubaliano ya Soko la Pamoja na Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki.

iii. Itahakikisha Zanzibar inakuwa mwanachama wa mashirika ya kimataifa kama FIFA, WHO na maeneo yote ambayo sio ya muungano.

iv. Itasimama imara na madhubuti kupinga vikali vitendo vyote vya ukandamizaji na uonevu dhidi ya Mataifa na watu wote ulimwenguni.

v. Itaendelea kuunga mkono ukombozi na uhuru wa nchi na watu wa Sahara Magharibi, Palestina, Rohinginya na mataifa na jamii nyengine zinazotawaliwa kwa mabavu na kupinga vikwazo vya kiuchumi vinavyowekwa kwa nchi kama Kyuba, Venezuela n.k.

vi. Itarejesha ari na msimamo madhubuti wa kuhakikisha Mshikamamo wa Umoja wa Afrika na maendeleo ya ukanda wa maziwa makuu na kusini mwa Afrika.

vii. Itapigania Bara la Afrika kuwa mwanachama katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN Security Council) na kupinga kura ya VETO katika Baraza hilo.

viii. Itashirikiana na serikali na wananchi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na mataifa mengine barani Afrika katika kulinda uhuru, amani, haki na rasilimali zao.

ix. Itaanzisha mashirikiano yenye manufaa ya pande mbili kwa kujiunga na Umoja wa BRICS na jumuiya nyingine zozote zenye mrengo na dhamira ya dhati ya kuwezesha ukombozi na maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kisayansi, kiteknolojia, kijeshi na kiutamaduni.

# 7. KULINDA MAZINGIRA NA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI



Kwa kuzingatia kuwa athari za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi ni makubwa sana, hali hii inatishia uendelevu wa Taifa katika uzalishaji wa chakula, afya na mabadiliko ya hali ya hewa kwa ujumla. Suala la kukabiliana na hali hii haliepukiki na linahitaji jitihada za pamoja za kiulimwengu.

Serikali ya ACT Wazalendo itaweka kipaumbele kwa kila sekta na kwa wananchi kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Hata hivyo, serikali ya ACT Wazalendo haitaruhusu, katika azma na jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya

tabia nchi, kuifanya Tanzania kuwa chambo na mlango wa kuingiza — ukoloni mpyall, ambao utawezesha kuendelea kwa shughuli za uzalishaji, zinazofanyika kwa uchafuzi mkubwa wa mazingira, kwa mataifa yaliyoendelea, huku sisi tukibaki na udumavu wa kiuchumi na kijamii, kwa kutojihusisha na shughuli za uzalishaji, kwa kutegemea mirabaha na maduhuli finyu yanayotokana na biashara ya hewa ukaa (kaboni/ carbon).

Kwa msingi huu, serikali ya ACT Wazalendo itafanya yafuatayo:

i. Itadhibiti biashara ya kaboni na kupitia upya mikataba ya biashara ya kaboni iliyopo na kuiweka wazi.

ii. Itahakikisha ulinzi wa mazingira kwa kuzingatia mikataba ya kimataifa, ikiwemo Mkataba wa Parisi [Paris Agreement], sheria za nchi na mbinu endelevu.

iii. Itahamasisha matumizi ya mbinu za asili na endelevu katika kulinda na kuhifadhi mazingira, kwa ajili ya sasa na vizazi vijavyo.

iv. Itaanzisha ushuru maalum kwa viwanda vikubwa, migodi na mashamba makubwa yanayochangia kiwango kikubwa cha uchafuzi wa mazingira.

v. Itaanzisha mfuko wa kulinda na kuhifadhi mazingira ili kuiongezea uwezo NEMC katika kusimamia utunzaji wa mazingira nchini.

vi. Itazisimamia kampuni za uzoaji taka katika mtaa kuzoa taka angalau mara moja kila wiki na kampuni itayoshindwa itafutiwa tenda yake.

vii. Itatengeneza dampo za kisasa na kutumia taka kama rasilimali za kutengenezea bidhaa kama mbolea na nishati mbadala.

viii. Itaanzisha Vituo vya Utabiri wa Hali ya Hewa [Climate Service Center] katika ngazi ya kila wilaya na kujenga mifumo ya kisasa wa kutoa tahadhari na taarifa ya hali ya hewa, kwa kushirikiana na sekta binafsi.

ix. Itaweka vivutio vya kikodi kwa viwanda vitakavyojiendesha kwa kutumia nishati safi, katika hatua mbali mbali za uzalishaji.

x. Itapunguza kodi na ushuru kwenye magari na vyombo vya moto vinavyotumia nishati safi, vinavyoingizwa nchini.

xi. Itaanzisha miundombinu ya uhifadhi wa mbegu za asili itakayosaidia kwenye kilimo ikolojia na utunzaji wa maarifa ya asili katika uzalishaji, kuboresha ustahimilivu wa wakulima na mazao dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi.

ACT Wazalendo

# TAIFA KWANZA LEO NA KESHO



ACT Wazalendo

**2025 - 2030**

# TAIFA LA WOTE, MASLAHI YA WOTE.